# JIHADI

## الجهاد

VITA VITAKATIFU KATIKA UISLAMU
UHALALI WAKE KISHERIA NDANI YA QUR'ANI

**Kimeandikwa na:**
Ustadh Murtadha Mutahhari

**Kimetarjumiwa na:**
Al Haj Ramadhani S. K. Shemahimbo

ترجمة

# الجهاد

## مشروعيّته فى القرآن

تأ ليف

مرتضى المطهري

من اللغة الإنجليزية  الى اللغة السوا حلية

**© Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
Al-Itrah Foundation

**ISBN No:** 978 - 9987 – 17 – 082 – 1

**Kimeandikwa na:**
Ustadh Murtadha Mutahhari

**Kimetarjumiwa na:**
Al Haj Ramadhani S. K. Shemahimbo

**Kimehaririwa na:**
Alhaj Hemedi Lubumba Selemani

**Kimepitiwa na:**
Mubarak A. Tila

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Novemba, 2014
**Nakala:** 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

# YALIYOMO


Neno la Mchapishaji ..................................................................... 1

**MLANGO WA KWANZA ........................................................ 2**

Maswali kuhusu Jihadi..................................................................... 2

Aya zenye shuruti na zenye amri kamili ........................................ 3

Je, tunaweza kupigana na Watu wote wa Kitabu wote .................. 6

Jizyah ni nini? ............................................................................... 8

Falsafa na Malengo ya Jihadi......................................................... 11

Uhalali wa Kisheria wa Jihadi ....................................................... 13

Amani sio utiifu ............................................................................ 14

Tofauti kati ya Uislamu na Ukristo ............................................... 17

Uislamu na Amani.......................................................................... 18

Masharti ya kupigana vita ............................................................. 18

Waislamu ndani ya Makka ............................................................ 20

**MLANGO WA PILI:....................................................................27**

Ni Ulinzi au Uchokozi ....................................................................27

Vipingamizi vya Ukristo kwenye Uislam .......................................27

Aya zenye amri kamili juu ya Jihadi ..............................................30

Aya zenye masharti ..........................................................................32

Kukimbilia kuwalinda Wanaoonewa ..............................................33

Vita vya Mwanzoni mwa Uislamu..................................................35

Kutafsiri Aya zenye amri kama za Masharti ..................................39

Hakuna kulazimishana katika Dini ..................................................39

Amani na Maafikiano.......................................................................45

**MLANGO WA TATU: ..................................................................49**

Ulinzi – Msingi wa Jihadi ...............................................................49

Aina za Ulinzi ..................................................................................49

Haki za Binadamu............................................................................51

Mgogoro Mdogo ........................................................................ 54

Tawhiid (Imani ya Mungu Mmoja) ni Haki binafsi
au ni ya Jumla? ........................................................................ 55

Kigezo cha Kutathmini Haki binafsi na Haki ya wote ................. 62

Uhuru wa Mawazo au Uhuru wa Imani? ...................................... 64

**MLANGO WA NNE: .................................................................. 66**

Suala la Utanguaji (ubatilishaji) .................................................. 66

Utanguaji (au ufutwaji) ................................................................ 66

Hakuna Ujumla bila kuwepo Upekee ........................................... 69

Ulinzi wa Maadili ya Ubinadamu ................................................. 72

Uhuru wa Imani, Fikra (Mawazo) ................................................ 74

Jizyah (aina ya Kodi) .................................................................. 76

بسم الله الرحمن الرحيم

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako kimetarjumiwa kutoka lugha ya Kiarabu na kuitwa, Jihadi. Kitabu hiki kimeandikwa na Ustadh Murtadha Mutahhari.

Jihad maana yake ni vita vitakatifu. Katika istilahi ya Kiislamu, Jihadi ni vita ambavyo hupiganwa kwa ajili ya kuitetea na kuilinda dini ya Mwenyezi Mungu. Jihadi ina taratibu na sheria zake, haipiganwi kiholela, kwani kwanza lazima ipatikane ruhusa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) au Imam wa zama au naibu wake.

Mwandishi katika kitabu hiki ameainisha masharti yote na mambo ya kuzingatiwa katika vita hivi vitakataifu na adabu zake.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu ambapo tunashuhudia vita kutoka kila mahali ulimwenguni na vingine vimepewa jina la Jihadi kinyume na masharti yaliyowekwa na dini ya Kiislamu.

Hivyo, taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu al-Haj Ramadhani S. K. Shemahimbo kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukitarjumi kitabu hiki kutoka Kiarabu. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin kisha Amin.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**

بسم الله الرحمن الرحيم

# MLANGO WA KWANZA:

## Maswali kuhusu Jihadi

قَـٰتِلُواْ ٱلَّذِينَ لَا يُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ وَلَا بِٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِ وَلَا
يُحَرِّمُونَ مَا حَرَّمَ ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥ وَلَا يَدِينُونَ دِينَ ٱلۡحَقِّ مِنَ
ٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلۡكِتَـٰبَ حَتَّىٰ يُعۡطُواْ ٱلۡجِزۡيَةَ عَن يَدٖ وَهُمۡ
صَـٰغِرُونَ ٢٩

**'Piganeni na wale wasiomwamini Mwenyezi Mungu wala siku ya Mwisho wala hawaharamishi aliyoharamisha Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, wala hawashiki Dini ya haki, miongoni mwa waliopewa Kitabu, mpaka watoe kodi kwa mkono hali wametii.'**
**(Qur'an 9:29)**

Aya hii ya Qur'ani inashughulika na Watu wa Kitabu, wale wasiokuwa Waislam wanaofuata mojawapo ya vitabu vitukufu, yaani, Wayahudi, Wakristo na pengine na Mazoroasti.

Aya inazungumzia kuhusu vita dhidi ya Watu wa Kitabu, lakini wakati huo huo haituambii tuwapige wote, inatuambia tuwapige wale tu ambao hawamwamini Mwenyezi Mungu na pia hawaamini juu ya Akhera, na wale ambao hawashikamani na amri za Mwenyezi

Mungu, wanaoruhusu kile alichokataza na wale ambao hawakujifunga kwenye dini ya haki. Ni watu hawa ambao tunapaswa kuwapiga mpaka walipe kodi (Jizyah). Ni kusema kwamba, wanapokuwa tayari kulipa Jizyah na wakaahidi kutokupanga njama dhidi ya Uislam, tunapaswa kuacha kupigana nao.

Aya hii inaibua maswali mengi ambayo yanahitaji kujibiwa kupitia uchunguzi wa aya za Qur'ani zinazohusiana na Jihadi, ambazo tutazitenga na kuzipitia.

Swali la kwanza linalojitokeza ni, ni nini hasa kinachomaanishwa na maneno haya: **'Piganeni na wale ambao hawamuamini Mwenyezi Mungu.'** Je maneno haya yana maana kwamba tupigane nao tangu mwanzoni kabisa? Au tupigane nao pale tu wanapopanga njama dhidi ya Dola ya Kiislam? Je, aya hii ni amri kamili, au inategemea kwenye tafsiri ya aya nyinginezo?

## AYA ZENYE SHURUTI NA ZENYE AMRI KAMILI

Kifungu hiki cha maneno ni muhimu sana, na ningependa nikielezee kwenu, kwani vinginevyo itakuwa ni vigumu kuzingatia ile maana kamili ya aya hii iliyoko kwenye mjadala. Amri yoyote (hata amri ya kibinadamu) inaweza ikatolewa mahali bila ya sharti, na halafu tena ikatolewa kwa namna nyingine pamoja na sharti lililoambatanishwa nayo. Katika hali hiyo, sisi mara moja tunatambua kwamba yeyote huyo aliyetoa amri hiyo na aliyeiweka sheria hiyo alitaka kufikia lengo moja katika hali zote mbili. Sasa basi, tukiwa tumekwisha kulitambua hili, tunapaswa kufanya nini? Je, tunapaswa kutii ile amri isiyo na sharti na kuchukulia kwamba ile yenye masharti ilitolewa kwa ajili ya hali hiyo maalum? Au tunapaswa kutafsiri zile aya ze-

nye amri isiyo na sharti kama zile zenye masharti, ambapo itamaanisha kushikamana na ile amri yenye masharti?

Ngoja nitoe mfano rahisi na mwepesi. Katika nyakati mbili tofauti kwa mfano, tunapewa amri na mtu ambaye ana mamlaka ya kufanya hivyo na ambaye tunaziheshimu amri zake. Katika wakati mmoja, tunaambiwa kwamba ni lazima tumheshimu mtu fulani, ambayo ni amri isiyo na sharti. Katika wakati mwingine, anatuamuru kufanya vivyo hivyo, akisema kwamba ni lazima tumheshimu mtu huyo kama akifanya jambo fulani, kama kushiriki kwenye mkutano wetu. Hii mara ya pili, amri hiyo ina tamko 'kama.' Amri sasa ni yenye masharti. Yule mtu aliyetoa amri hiyo hakusema tu kwamba mtu fulani anapaswa kuheshimiwa. Amri ya awali haikuwa na sharti; tuliambiwa tu kwamba tumheshimu, na kwa kuchukulia kwamba tunayo masikio na tuliisikia amri hii, kwetu ingekuwa na maana kwamba tulipaswa kumheshimu mtu yule, sawa awe amekuja kwenye mkutano wetu ama alikuwa mvivu sana wa kulijali hilo. Lakini pale tunaposikia hii amri nyingine, tunaelewa kwamba tunapaswa kumheshimu mtu huyo pale tu anapokuja kwenye mkutano wetu, na kama akishindwa kufanya hivyo, basi hatupaswi kumheshimu.

Ulamaa wanasema kwamba utaratibu unatutaka sisi kutafsiri zile aya zenye amri isiyo na sharti kama zile zenye masharti, kwa maana kwamba ni lazima tuchukulie lile lengo la aya zenye amri isiyo na sharti kuwa ni sawa na zile zenye masharti.

Sasa, miongoni mwa aya za Qur'ani zenye amri isiyo na sharti, pia zenye kuhusiana na Jihadi ni inayosema:

قَـٰتِلُواْ ٱلَّذِينَ لَا يُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ وَلَا بِٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِ

وَلَا يُحَرِّمُونَ مَا حَرَّمَ ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥ ﴿٢٩﴾

**‘Piganeni na wale wasiomwamini Mwenyezi Mungu wala siku ya Mwisho wala hawaharamishi aliyoharamisha Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.....’ (9:29).**

Katika aya nyingine tunaambiwa:

وَقَٰتِلُواْ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ ٱلَّذِينَ يُقَٰتِلُونَكُمۡ

**’Na piganeni katika nji ya Mwenyezi Mungu na wale wanaowapiga..’ (2:190)**

Ni nini maana ya aya hizi? Je, zina maana kwamba ni lazima tupigane na watu hawa bila kujali iwapo kwamba wanataka kutushambulia sisi? Je amri yenyewe haina shuruti hivyo kwamba ni lazima tupigane nao, iwe wananuia kutushambulia ama hapana, iwe wana hatia ya uchokozi ama hapana?

Kuna maoni yenye uwezekano ya namna mbili. Moja ni kwamba amri hiyo inabaki kuwa ni kamili isiyo na sharti. Watu wa Kitabu sio Waislamu, hivyo tunaruhusiwa kuwapiga. Tunaruhusiwa kupigana na wasio Waislam hadi tuwashinde. Kama sio Waislam wala sio Watu wa Kitabu, tunapaswa kuwapiga mpaka ama wawe Waislamu au tuwauwe wote. Kama ni Watu wa Kitabu, basi tunapaswa kupigana nao mpaka wawe Waislamu, au kama hawawi Waislamu, basi mpaka watulipe kodi ya Jizyah. Hayo ndio maoni ya wale wanaosema kwamba aya hiyo inabakia kuwa yenye amri kamili isiyo na sharti.

Hayo maoni mengine, hata hivyo, yanashikilia kwamba hizo aya zenye amri kamili lazima zitafsiriwe kama zile zenye masharti. Mtu mwenye mawazo kama haya atasema hizo aya nyingine za Qur’ani zinatuletea masharti kwa ajili ya uhalali wa Jihadi, tunatambua

kwamba maana halisi ya aya hizo sio zisizo na masharti hata kidogo. Ni yapi basi masharti kwa ajili ya uhalali wa Jihadi? Miongoni mwao kwa mfano, ni haya yafuatayo: Kwamba upande wa pili unadhamiria kutushambulia; au kwamba unajenga mpaka dhidi ya wito wa Uislamu, kwa maana kwamba unakanusha uhuru wa wito huo na unakuwa ni kikwazo kwenye ueneaji wake, wakati ambapo Uislamu unasema kwamba vikwazo hivyo ni lazima viondolewe. Au, kadhalika katika suala la watu wanaopatwa na uonevu na ukandamizaji wa kikundi cha watu kutoka miongoni mwao, Uislamu unasema kwamba ni lazima tupigane na wakandamizaji hao ili kuwatoa wanaoonewa kutoka kwenye makucha ya ukandamizaji. Hili limeelezewa ndani ya Qur'ani hivi:

وَمَا لَكُمْ لَا تُقَـٰتِلُونَ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱلْمُسْتَضْعَفِينَ .....

**"Na mna nini hampigani katika njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanaoonewa....." (4:75)**

Ni kwa nini kwamba hatupigani kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kwa ajili ya wanaume, wanawake na watoto ambao wanapatwa na mateso na ukandamizwaji? Ili kupata majibu ya swali hili, tunapaswa kuzichunguza aya zote za Qur'ani ambazo zinahusiana na Jihadi.

## JE, TUNAWEZA KUPIGANA NA WATU WA KITABU WOTE?

Swali la pili linahusiana na ukweli kwamba aya yenyewe haielezi wazi kabisa kwamba tunapaswa kupigana na Watu wa Kitabu wote,

bali inatueleza kwamba tupigane dhidi ya wale ambao hawamwamini Mwenyezi Mungu wala juu ya Akhera.... ambao kile alichokikataza Mwenyezi Mungu wao wanachukulia kuwa kinaruhusiwa (ni halali) na ambao kabisa hawajashikamana na dini yoyote ile ya haki. Sasa, hii inamaanisha nini? Je, ina maana kwamba Watu wa Kitabu wote jumla (Wayahudi wote, Wakristo na wafuasi dini tofauti tofauti) hawana imani juu ya Mwenyezi Mungu, hawaamini Akhera, hawaamini sheria za Mwenyezi Mungu na hawana imani juu ya dini yoyote iliyoko katika misingi ya haki, hivyo kwamba kama mmoja wao atadai kwamba anamwamini Mwenyezi Mungu ni muongo na kwa kweli hamwamini Mwenyezi Mungu? Hivi Qur'ani hasa inasema kwamba Watu wa Kitabu wote, licha ya madai yao kwamba wanamwamini Mwenyezi Mungu, kwa uhalisia hasa hawana imani kama hiyo? Je inawezekana kwetu sisi kuhoji kwamba kwa sababu Wakristo wanadai kwamba Yesu ni Mungu au 'Mwana wa Mungu' ni kweli kwamba hawana imani juu ya Mwenyezi Mungu? Au kwamba wale wanaosema **'Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba' (5:64)** hawawezi kuwa wenye kuamini katika Mungu wa kweli na je hilo linawahusu Watu wa Kitabu wote waliobakia?

Kufikiri katika namna hii kutakuwa na maana kwamba sisi tunaamini kwamba Qur'ani haitambui imani yoyote juu ya Mwenyezi Mungu au ufufuo zaidi ya ile imani ya Waislam. Kama tukiulizwa ni kwa nini, tutasema kwamba Qur'ani inaelezea imani za Watu wa Kitabu zimekanganyika na kueleweka visivyo. Mkristo, hata kama akiwa ni mwanachuoni msomi wa Kikristo anamtambua Mungu na pia anautambua Upweke wa Mwenyezi Mungu, lakini wakati huo huo anaweza akawa na maoni kuhusu Yesu au Mariam ambayo yanachafua imani yake katika Upweke wa Mwenyezi Mungu (*Tawhiid*). Haya ndio maoni ya baadhi ya wafasiri wa Qur'ani. Kwao wao, pale Qur'ani inapotuambia tunapaswa kupigana na Watu wa Kitabu, ina maana ya kutuambia tupigane na Watu wa Kitabu

wote, kwamba imani juu ya Mwenyezi Mungu ya yoyote kati yao sio imani sahihi; kwamba imani juu ya ufufuo na katika nini Mwenyezi Mungu amekikataza na kuruhusu kipi, ya yoyote kati yao sio sahihi. Wanachokiamini wafasiri hawa ni kwamba neno 'Mtume' katika aya hii lina maana ya huyu mwisho wa Mitume Muhammad (s.a.w.w.), na kwamba 'dini ya haki' lina maana ya dini ambayo binadamu wa zama hizi wana wajibu wa kuikubali, badala ya dini ambayo ilikuwa ni wajibu kuikubali wakati wa kipindi fulani huko nyuma.

Kikundi kingine tofauti cha wafasiri hata hivyo, kinachukulia kwamba kwa kauli au maelezo haya, Qur'ani inakusudia kutuonyesha kwamba Watu wa Kitabu wanaunda makundi ya namna mbili; kwamba sio kama wote wanafanana sawa; kwamba baadhi yao kwa kweli wanamuamini Mwenyezi Mungu na ufufuo, ni kweli wanaamini katika sheria za Mwenyezi Mungu. Hivyo, sisi hatuna la kufanya juu yao. Wale ambao tunapaswa kupigana nao ni wale ambao ni Watu wa Kitabu kwa jina tu, lakini kwa uhalisia wao hawana imani sahihi hata kidogo, na ambao hawachukulii kama ni haramu kile alichokikataza Mwenyezi Mungu, hata kile alichokikataza ndani ya dini yao wenyewe. Hivyo sio kwamba tunapaswa kupigana na Watu wa Kitabu wote, bali kikundi kutoka miongoni mwao. Hili, kwa lenyewe ni suala jingine kabisa.

## JIZYAH NI NINI?

Swali la tatu linahusiana na neno jizyah au kodi. Tunaambiwa tupigane nao hadi pale watakapolipa hiyo jizyah, ambayo ina maana kwamba mpaka ama waukubali Uislam au kulipa jizyah. Ndani ya Qur'ani hakuna shaka kwamba tofauti imetajwa kati ya Watu wa Kitabu na washirikina, wale ambao rasmi wanaabudu masanamu na

hawafuati kitabu chochote kitakatifu cha ki-Mungu. Hakuna mahali popote ndani ya Qur'ani ambapo tunaambiwa tupigane na washirikina mpaka walipe jizyah, na kwamba tusiendelee kuwapiga mara pale wanapokuwa wamelipa jizyah hiyo. Kuhusu Watu wa Kitabu hata hivyo, tunaambiwa kwamba pale wanapokuwa wamehiari kulipa jizyah tusiendelee kupigana nao tena. Hii ni tofauti ambayo ipo kwa dhahiri kabisa.

Hii inatufikisha kwenye swali: *Jizyah* ni nini? Kuna mjadala kuhusu neno lenyewe. Baadhi wanasema hilo sio neno la Kiarabu kwa asili, yaani halina mzizi wa Kiarabu, lakini ni neno linalozalika kutoka kwenye neno la Kiajemi *Gaziyet*, jina la kodi ilioanzishwa na Anoushiravan, aliyekuwa Mfalme wa Sassania wa Kiajemi. Kodi hii hata hivyo, ilikuwa ni kodi ya kichwa juu ya watu wa Uajemi wenyewe na sio kwa mwingine yoyote yule, na ilikuwa ikikusanywa kwa ajili ya vita. Matumizi ya neno hilo ndipo yakaenea kutoka Iran hadi Hira, mji ulioko kwenye maeneo ya Najaf ya sasa (huko Iraqi) na kutokea hapo likatwaliwa na Ghuba ya Arabuni yote ambako lilitumika kwa mapana kabisa.

Kuna wengine wanaolikataa hili. Ingawa ni kweli kwamba neno *jizyah* na *gaziyeh* yanafanana kwa karibu sana, *jizyah* ni neno la Kiarabu kutokana na mzizi '*Jaza*' – na haya ndio maoni ya wanaetimolojia (elimu ya asili na historia na maneno) walio wengi. Tunachokipenda hasa hapa sio asili ya neno hata hivyo, kwani kile tunachotafuta ni asili na msingi ambao unaashiriwa na neno lenyewe. Je, jizyah hiyo ni utozaji wa 'pesa ya ulinzi' au namna ya kutishia usalama wa mtu (usaliti - *blackmail*)? Je, Uislamu unatuambia sisi tupigane ili tupate pesa kwa kutishia, na wakati zikishalipwa tusiendelee kupigana? Mshairi mmoja anasema:

> ‘Sisi ni wa namna kwamba, kutoka kwa wafalme tumechukua kodi,
>
> Baada ya kuwa tumechukua mataji yao na fimbo zao zilizo rasmi’

Kama maana ya jizyah inarejelea kwenye namna ya tozo la vitisho (blackmail), swali linaibuka kwamba ni nini maana yake yote hasa. Ni maelekezo ya namna gani hayo? Hiyo sio sheria ya mabavu na nguvu za kikatili?

Itakuwa na msingi gani katika haki za binadamu na sheria, kwa Uislam kuwapa Waislam ruhusa, hata kufanya ni wajibu juu yao kupigana na watu wa dini nyingine mpaka ama waukubali Uislamu au kuwahonga Waislamu? Njia zote hizi mbadala zinaleta tatizo, kwani kupigana nao mpaka wakubali Uislamu itakuwa ni kuulazimisha Uislamu juu yao, na kupigana nao mpaka wawahonge Waislamu itakuwa ni kuwachuma, ni kuchukua mali kutoka kwao. Njia zote mbadala ni matumizi ya ukatili na nguvu, kwani ama ina maana ya kulazimisha imani juu yao au kuchukua mapesa kwa nguvu kutoka kwao. Kwa hiyo hapa pia ni lazima tuingie kwenye maelezo ya kina ili kuweza kujua ni nini hasa hii jizyah. Je kweli ni ‘kuwabana kwa vitisho (blackmail),’ ni ‘pesa ya ulinzi’ ni ‘malipo ya fidia? Au ni kitu kingine kabisa?

Hapa Qur’ani inasema: ‘**wahum swaghiruun**’ kwa maana kwamba ‘na wao ni wadogo’ – wakati wao ndio wadogo – *Swaghiruun* inakuja kutokana na neno ‘*Sighar*’ na hili maana yake ni chini (ndogo). Nini maana ya: wao ndio wadogo? Hili vilevile ndio swali la nne. Ni nini maana ya – wao ndio wadogo/wa chini? Je ina maana kwamba wao ni lazima wanyenyekee mbele ya nguvu zenu au Uislamu una maana nyingine mbali na unyenyekevu (kuwa mnyenyekevu)? Hapa tunaweka pembeni

maana ya aya hii na maswali yanayojitokeza kutokana nayo, na tuangalie mambo mengine ambayo ni lazima yachambuliwe tofauti na kujadiliwa.

## FALSAFA NA MALENGO YA JIHADI

Suala la tano linahusiana na sababu ya sheria ya Jihadi katika Uislamu. Wengine wanaamini kwamba kusingekuwa na Jihadi katika dini kabisa: dini isiwe na sheria ya vita kwa sababu vita ni jambo baya, dini ni lazima iipinge vita na sio yenyewe iweke vita kama ni sheria. Sisi kwa upande mwingine, tunajua kwamba Jihadi ni kanuni ya msingi katika Uislamu.

Kati ya hoja ambazo kwamba Wakristo wanatangaza katika mtindo usio wa kawaida dhidi ya Uislamu, mojawapo ni hii. Kwanza wanauliza kwa nini sheria kama hiyo imo ndani ya Uislamu? Kisha wanaeleza kwamba, kutokana na ruhusa hii ya kisheria, Waislamu walianzisha vita na ummah kadhaa na kuulazimisha Uislamu juu yao. Wao wanadai kwamba Jihadi za Kiislamu zote zilipiganwa kwa ajili ya ulazimishaji wa imani ya Kiislamu. Ni kutokana na ruhusa hii kwamba Waislamu waliulazimisha Uislamu kwa mabavu, ambavyo ndio namna, kama wanavyosema wao, mpaka sasa Uislamu umekuwa ukienea siku zote. Wanasema kwamba sheria ya jihadi katika Uislamu na moja ya haki za binadamu, yaani uhuru wa kuamini, viko kwenye mgongano wa milele. Hili ni moja ya mambo ya kujadiliwa.

Jambo la pili ni tofauti ambayo Uislamu imeidumisha katika sheria za Jihadi baina ya washirikina na wasiokuwa washirikina. Kuna kanuni yenye kubainisha kwa ajili ya kuishi kwa maelewano na Watu wa Kitabu ambayo haitumiki kwa washirikina.

Jambo jingine ni iwapo kama Uislamu unatofautisha kati ya Ghuba ya Uarabuni na sehemu nyingine ya dunia iliyobakia. Je, Uislamu umejiteulia wenyewe mahali kwa ajili ya Makao yake Makuu, kituo chake, ambamo hakuna yeyote miongoni mwa washirikina au Watu wa Kitabu anayeruhusiwa kuingia humo? Na je, mahali hapo ni Ghuba ya Arabuni, ambapo kwamba katika maeneo mengine Uislam sio mkali kiasi hicho, na kwa mfano, huko wanaishi kwa maelewano pamoja na washirikina au Watu wa Kitabu? Kwa kifupi, Ghuba ya Arabuni ina tofauti yoyote katika hali hizi au hapana? – Jibu ni kwamba kati ya Makkah na sehemu nyinginezo bila shaka kuna tofauti, na katika aya iliyotangulia hii iliyoko kwenye mjadala tunaambiwa kwamba:

..... إِنَّمَا ٱلْمُشْرِكُونَ نَجَسٌ فَلَا يَقْرَبُوا۟ ٱلْمَسْجِدَ ٱلْحَرَامَ بَعْدَ عَامِهِمْ هَـٰذَا

**'Enyi mlioamini! Hakika washirikina ni najisi, kwa hiyo wasiukaribie Msikiti Mtakatifu (ulioko Makkah).....' (9:28)**

Jambo la nne linahusiana na mapatano na washirikina. Je Mwislamu anaruhusiwa kufanya mapatano na watu kama hao? Anaweza kuwekeana ahadi nao? Na kama akifanya hivyo, je makubaliano hayo yanapasa kuheshimiwa au hapana?

Jambo la mwisho linahusiana na masharti ya vita. Wakati Uislamu ukiwa umehalalisha mambo ya kivita, ni aina gani ya vita, kwa maana ya masharti maalum ya vita, je, Uislamu unaona ni halali, na ni aina gani ya vita ambavyo inaviona kama vilivyokatazwa? Kwa mfano, Uislamu unaona kwamba kuua umati mkubwa wa watu kuwa kisheria ni halali au imekatazwa? Je, Uislamu unaona kwamba inaruhusiwa kuwauwa wale ambao hawakunyanyua panga; wanawake

wazee. Watoto, wanaume ambao kwa amani kabisa wanashughulika na kazi na biashara zao? Kuwauwa wote hawa, kwa mujibu wa maoni ya Uislamu kunaruhusiwa ama kunakatazwa? Haya ni mambo ambayo yote yanapasa kujadiliwa. Aya zinazohusiana na Jihadi zinajitokeza katika mahali pengi ndani ya Qur'ani. Tutajaribu kuzikusanya zote kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, ili tuweze kuyapata maoni ya Uislamu juu ya suala hili.

## UHALALI WA SHERIA YA JIHADI

Jambo la kwanza ambalo tutaliangalia linahusu uhalali wa Sheria ya jihadi. Je, ni sahihi sheria ya vita kuwemo katika muktadha wa kidini na maandiko ya amri zake? Wapinzani wanasema: "Hapana, vita ni uovu, na dini lazima wakati wote ipinge vita. Ni lazima wakati wote itetee na kuunga mkono amani. Na kwa vile inadhamiria kutetea amani, ni lazima isiwe na sheria yoyote kuhusu vita, na yenyewe kamwe isitoke kwenda vitani." Hii ndio aina ya propaganda ambayo Ukristo unaiendesha, dhaifu na nyeupe kabisa isiyo na msingi wala msimamo.

Hivi vita wakati wote ni mbaya? Kama ikiwa ni katika kutetea haki, dhidi ya muonevu, bado ni mbaya tu? Ni wazi kabisa kwamba kwa hali hiyo sio mbaya. Ni lazima tuziangalie hali na sababu za vita na tuangalie ni kwa sababu na lengo gani vita vinapiganwa. Kuna nyakati ambapo vita ni uchokozi. Wakati kwa mfano, kundi la watu ama taifa likikodolea macho ya ulafi kwenye haki za wengine, kwenye ardhi za wengine, au linapotupia macho mali za kawaida za watu, au linakuwa mateka wa shauku, kutamani cheo au ubora na kudai kwamba: "Kati ya mbari (utaifa) zote, mbari yetu ndio maarufu na bora kuliko zote, na kwa hiyo sisi lazima tutawale mbari zote zile." Ni wazi kabisa kwamba vita kwa ajili ya sababu hizi sio

halali. Wakati vita vinapopiganwa kutwaa ardhi, kukamata umiliki wa utajiri wa taifa, au kwa ajili ya kuwatweza wengine na kutokana na hisia za ubaguzi wa kimbari (yaani kusema ‘wale watu ni duni kwetu, sisi ni wabora, na wabora lazima watawale juu ya madhalili), hivyo ni vita vya uchokozi. Aina za vita kama hizi kwa kweli ni za kiovu, na hapawezi kuwa na shaka juu ya hilo. Tutazungumzia juu ya aina nyingine ya vita, vile vita vya kuweka masharti au kulazimisha imani.

Lakini kama vita vya utetezi vinapiganwa katika kukabiliana na uchokozi, watu wamekalia ardhi yetu, au wamekodolea macho yao kwenye mali na utajiri wetu, au juu ya uhuru na heshima ya kujitukuza kwetu, ambavyo wanataka kutunyang’anya, na wanadhamiria kulazimisha utawala wao juu yetu, katika hali kama hizi, dini ina lipi la kusema? ‘Ni wazi kabisa kwamba vita ni uovu, kushika silaha ni uovu, kunyanyua upanga ni uovu,’ na kwamba inatetea amani? Na, wakati tunapokabiliwa na shambulizi linalotarajiwa kutokeza, na shambulizi la kuangamizwa, je, hatupaswi kwenda vitani? Kama hatupaswi, hiyo haitamaanisha kushindwa kujitetea na kujilinda wenyewe kwa kisingizio cha amani? Hii haitakuwa ni amani, huku kutakuwa ni kusalimu amri.

## AMANI SIO UTIIFU

Katika tukio kama hilo, hatuwezi kusema kwamba kwa sababu sisi ni watetezi wa amani, tunapingana na vita. Jambo kama hilo litakuwa na maana kwamba sisi ni watetezi wa mateso, watetezi wa kusalimu amri. Usifanye kosa lolote, amani na kujisalimisha vinatofautiana kama chaki na jibini. Maana ya amani ni kuishi kwa pamoja kwa heshima kabisa, lakini kujisalimisha sio maisha ya pamoja yenye

heshima; ni maisha ya pamoja ambayo kwa upande mmoja hayana heshima kabisa. Kwa kweli, ni maisha ya pamoja ambayo kabisa hayana heshima kwa pande zote. Kwa upande mmoja, fedheha ni ya maonevu, na kwa upande mwingine ni fedheha ya kujisalimisha mbele ya dhalimu, mbele ya dhuluma na ukandamizaji.

Hivyo dhana hii potofu ni lazima ifutwe, na mtu ambaye anapinga vita, akisema kwamba vita moja kwa moja ni mbaya , iwe ya kidhalimu ama ya ulinzi na upinzani dhidi ya udhalimu, atakuwa amefanya kosa kubwa sana. Vita ambavyo vina maana ya uchokozi ni lazima vishutumiwe na kulaaniwa kabisa, ambapo vita ambavyo ni vya upinzani (qiyam) dhidi ya uvamizi sio vya kushutumiwa na ni vya muhimu kwa ajili ya maisha ya binadamu.

Qur'ani pia inadokezea jambo hili, kwa kweli hasa inaliangazia hili. Inasema hivi:

..... وَلَوْلَا دَفْعُ ٱللَّهِ ٱلنَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَّفَسَدَتِ ٱلْأَرْضُ .....

**".....Na kama Mwenyezi Mungu asingeliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, ingeliharibika ardhi....." (2:251)**

..... لَّهُدِّمَتْ صَوَٰمِعُ وَبِيَعٌ وَصَلَوَٰتٌ وَمَسَٰجِدُ يُذْكَرُ فِيهَا ٱسْمُ ٱللَّهِ كَثِيرًا

**".....basi yangekivunwa mahekalu na makanisa na (sehemu) za kuswalia na misikiti ambayo ndani yake hutajwa jina la Mwenyezi Mungu kwa wingi....." (22:40).**

Hivyo kama Mwenyezi Mungu asingewazuia baadhi ya watu kwa njia ya wengine, uharibifu na dhulma vingekuwa ndio vinatawala kila mahali. Kadhalika, ni kwa sababu hii kwamba nchi zote za dunia zinaiona kwamba ni muhimu, ni lazima juu yao kutayarisha majeshi yenye silaha kwa ajili ya ulinzi wao. Kuwepo kwa majeshi ya kivita, ambayo wajibu wao ni kuzuia uvamizi ni hitajio la muhimu kabisa. Sasa, kama hizi ni nchi mbili ambazo zote zina majeshi ya kivita, moja kwa ajili ya uchokozi na jingine kwa ajili ya ulinzi, usiseme kwamba ile nchi yenye jeshi bila nia ya uchokozi ni dhaifu zaidi kuliko hiyo nchi nyingine, na kwamba kama ingekuwa na nguvu zaidi, nayo pia ingekusudia kufanya uchokozi. Hatuhusiki na jambo hili. Ukweli ni kwamba uwepo wa jeshi kwa ajili ya ulinzi ni lazima kwa kila nchi kwa ajili ya taifa hilo kuwa na nguvu za kutosha kuzuia uchokozi wowote dhidi yake.

Hivyo Qur'ani inatuambia:

وَأَعِدُّواْ لَهُم مَّا ٱسْتَطَعْتُم مِّن قُوَّةٍ وَمِن رِّبَاطِ ٱلْخَيْلِ
تُرْهِبُونَ بِهِۦ عَدُوَّ ٱللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ .....

**"Na waandalieni nguvu kama vile muwezavyo, na kwa farasi waliofungwa, ili mumtishe adui wa Mwenyezi Mungu na adui yenu....." (8:60).**

Kauli hii ina maana kwamba, "Andaeni majeshi kwa kiasi mtakavyoweza, na yawekeni majeshi yenu kwenye mipaka yenu. *Ribat* linakuja kutokana na neno *Rabt*, ambalo lina maana ya kufunga. *Ribat-il-Khayl* maana yake ni kufunga farasi (waliofungwa kwenye

vigingi). Kauli kuhusu farasi kuwa tayari imetolewa kwa sababu hapo zamani, nguvu ya majeshi ilikuwa hasa ni kuwa na farasi, lakini kwa kawaida kila zama ina sifa zake. Kile inachokisema Qur'ani hapa ni kwa ajili ya hofu ya nguvu zetu kuingia kwenye nyoyo za maadui zetu na ili wasiwe na mawazo ya uchokozi katika akili zao, ni lazima tujijengee wenyewe jeshi imara na tufanye tuwe na nguvu.

## TOFAUTI KATI YA UISLAMU NA UKRISTO

Inasemekana kuhusu Ukristo kwamba hauna uwazi wa kutokuwa na kanuni yoyote inayotawala vita. Sisi kwa upande mwingine tunasema kwamba Uislamu una sifa ya wazi ya kuwa na sheria ya Jihadi. Kama tukiangalia kwa ukaribu wa makini kabisa tunaona kwamba katika Ukristo hakuna jihadi kwa sababu wenyewe hauna chochote kabisa. Ambapo kwa hili ni maana ya kwamba hakuna muundo wa kijamii wa Kikristo, hakuna mfumo wa kisheria, na hakuna kanuni za ki-Kristo za ni namna gani jamii iundwe. Hakuna haja ya dini hii kuwa na sheria ya jihadi. Ukristo hauna zaidi ya mafundisho machache ya kimaadili ambayo yanaunda seti ya ushauri kama vile "sema kweli," "usiseme uongo," "usile kwa pupa mali za wengine" na kadhalika. Dini kama hiyo haina mwito wa jihadi. Uislamu hata hivyo ni dini ambayo inaona kwamba ni wajibu na dhima yake kuunda dola ya Kiislamu.

Uislamu umekuja kurekebisha jamii na kuunda taifa na serikali. Agizo lake ni kurekebisha ulimwengu wote. Dini kama hiyo haiwezi kuwa yenye kupuuza na kutojali kuelekea kwenye maendeleo mbalimbali. Haiwezi kutokuwa na sheria ya jihadi. Kwa namna hiyo hiyo, serikali yake haiwezi kutokuwa na jeshi. Wakati upeo wa Ukristo umewekewa mipaka mno, ule wa Uislamu uko mpana mno. Wakati Ukristo hauvuki mipaka ya ushauri, Uislamu ni dini

ambayo inazingatia shughuli zote za maisha ya binadamu. Unazo sheria zinazosimamia jamii; sheria za kiuchumi, na sheria za kisiasa. Ulikuja kuanzisha dola na kuunda serikali. Mara hili litakapokamilika, utabakia vipi bila ya kuwa na jeshi? Ni vipi utakuwa bila ya sheria ya jihadi?

## UISLAMU NA AMANI

Hivyo, yale makundi yanayodai kwamba dini lazima wakati wote ipinge vita, na kutetea amani, kwa sababu amani ni nzuri na vita ni mbaya kabisa moja kwa moja, wao wanakosea. Dini bila shaka ni lazima itetee amani, na Qur'ani inasema: 'Wa sulhu khayrun' yaani 'amani ni bora' lakini ni lazima vilevile itetee vita. Kama ule upande wa upinzani hauko tayari kuishi pamoja kwa kuheshimiana, kwa mfano, na ukiwa na uonevu unanuia kuikanyaga heshima na hadhi ya binadamu, na sisi tukanyenyekea, basi tutakuwa tumekaribisha mateso, tumekubali udhalili. Uislamu unasema:

> 'Fanyeni amani kama ule upande mwingine uko tayari kuikubali. Laa sivyo, nao ukageukia kwenye vita, basi piganeni vita.'

## MASHARTI YA KUPIGANA VITA

Jambo la pili linahusiana na mazingira ambamo Uislamu unasema lazima tupigane vita. Aya ya kwanza ya Qur'ani ambayo ilishushwa kuhusu jihadi, kwa maoni yanayokubaliwa na wafasiri wote, ni ile ambayo ipo kwenye Surat Hajj"

۞ إِنَّ ٱللَّهَ يُدَٰفِعُ عَنِ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ خَوَّانٖ كَفُورٍ ٣٨
أُذِنَ لِلَّذِينَ يُقَٰتَلُونَ بِأَنَّهُمۡ ظُلِمُواْۚ وَإِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ نَصۡرِهِمۡ لَقَدِيرٌ ٣٩ ٱلَّذِينَ
أُخۡرِجُواْ مِن دِيَٰرِهِم بِغَيۡرِ حَقٍّ إِلَّآ أَن يَقُولُواْ رَبُّنَا ٱللَّهُۗ وَلَوۡلَا دَفۡعُ ٱللَّهِ ٱلنَّاسَ
بَعۡضَهُم بِبَعۡضٖ لَّهُدِّمَتۡ صَوَٰمِعُ وَبِيَعٞ وَصَلَوَٰتٞ وَمَسَٰجِدُ يُذۡكَرُ فِيهَا ٱسۡمُ ٱللَّهِ
كَثِيرٗاۗ وَلَيَنصُرَنَّ ٱللَّهُ مَن يَنصُرُهُۥٓۚ إِنَّ ٱللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ٤٠ ٱلَّذِينَ إِن
مَّكَّنَّٰهُمۡ فِي ٱلۡأَرۡضِ أَقَامُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَوُاْ ٱلزَّكَوٰةَ وَأَمَرُواْ بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَنَهَوۡاْ
عَنِ ٱلۡمُنكَرِۗ وَلِلَّهِ عَٰقِبَةُ ٱلۡأُمُورِ ٤١

**"Hakika Mwenyezi Mungu huwakinga walioamini. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila haini, mwenye kukufuru sana. Wameruhusiwa kupigana vita kwa sababu wamedhulumiwa. Na kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia. Wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, ila tu kwa kuwa wanasema Mola Wetu ni Mwenyezi Mungu. Na lau Mwenyezi Mungu asingewakinga watu kwa watu, basi yangelivunjwa mahekalu na makanisa na (sehemu) za kuswalia na misikiti ambyo ndani yake hutajwa jina la Mwenyezi Mungu kwa wingi. Na hakika Mwenyezi Mungu humnusuru yule anayemnusussru Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye enzi. Wale ambao tukiwamakinisha katika ardhi husimamisha swala na wanatoa Zaka na wakaamrisha mema na wakakataza mabaya. Na kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo ya mambo yote" (Qur'an 22:38-41)**

Hizi ni aya zenye kustaajabisha kabisa. Ndio aya za kwanza kabisa kushushwa kuhusiana na sheria za jihadi.

# WAISLAMU NDANI YA MAKKA

Kabla ya uchanganuzi juu aya hizi, hata hivyo, ni lazima tugeuze mazingatio yetu kwenye jambo jingine kabisa kwanza. Kama tunavyojua, wahyi wa kwanza ulileta kwa Mtukufu Mtume huko Makka, wakati yeye alipokuwa na umri wa miaka arobaini. Baada ya hapo, Bwana Mtume (s.a.w.w.) aliishi mjini Makka kwa muda wa miaka kumi na tatu, katika muda ambao, ama yeye mwenyewe au masahaba zake waliteswa sana na wapagani wa ki-Kuraishi, nyumba zilizokuwa zinatawala mjini Makka, kwa kiasi ambacho kikundi miongoni mwao walilazimika kuomba ruhusa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ya kuhama. Waliondoka Makka na wakaenda hadi Ethiopia. Kwa kurudia mara kwa mara, Waislam waliomba ruhusa kwa Mtukufu Mtume ya kujilinda wenyewe, lakini katika kipindi hicho cha miaka kumi na tatu ambayo yeye alikuwa mjini Makka, yeye hakuwapa ruhusa hiyo, ambavyo kwayo kulikuwa na sababu nzuri tu, mpaka hatimaye kazi yake tukufu ilipofikia hatua fulani ya maendeleo yake na Uislamu ukaenea kwenye maeneo mengine, na Madina. Huko, kikundi kidogo cha wakazi wa Madina kiliingia kwenye Uislamu (kilisilimu) na kuchukua kiapo cha utii kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na wakafunga mkataba kwamba kama yeye atakuja Madina wao watamuunga mkono na kumsaidia. Hivyo Mtukufu Mtume akahamia Madina na Waislamu pia nao, kidogo kidogo wakahamia huko, na huko Madina, kwa mara ya kwanza kabisa ngome huru ya Kiislamu ikaanzishwa. Katika mwaka wa kwanza, ruhusa kwa ajili ya kujilinda ilikuwa bado haijatolewa. Ilikuwa ni katika mwaka wa pili hijiria ambapo aya za kwanza juu ya Jihadi, hizo nilizozitaja hapo juu, zikawa zimeshushwa. Mwelekeo wa aya hizi unakuja hivi:

۞ إِنَّ ٱللَّهَ يُدَٰفِعُ عَنِ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ

**“Hakika Mwenyezi Mungu huwakinga walioamini.” (Qur’an 22:38)**

Hii inaashiria kwamba washirikina walikuwa ni mahaini kwa Waislam, waliwasaliti, na wakafanya uchokozi dhidi yao, na waliikataa rehema ya Mwenyezi Mungu juu yao wenyewe. Kisha Qur’ani inatamka:

أُذِنَ لِلَّذِينَ يُقَٰتَلُونَ بِأَنَّهُمۡ ظُلِمُواْۚ

**”Wameruhusiwa (kupigana) wale wanaopigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa.....” (Qur’an 22:39)**

Ruhusa ya kupigana imetolewa kwa wale ambao watu wengine wamekuja kuwapiga. Ambayo ina maana kwamba: Enyi Waislamu, sasa kwa vile washirikina wenye kukufuru wamekuja kukupigeni, basi wapigeni. Kwa uhalisia hii ni kauli ya ulinzi. Kwa nini ruhusa hii imetolewa? Kwa sababu wale wanaoonewa ni lazima wajilinde wenyewe. Kisha inafuatia ahadi ya msaada:

وَإِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ نَصۡرِهِمۡ لَقَدِيرٌ ٣٩ ٱلَّذِينَ أُخۡرِجُواْ مِن دِيَٰرِهِم

بِغَيۡرِ حَقٍّ إِلَّآ أَن يَقُولُواْ رَبُّنَا ٱللَّهُ

**“.....Na kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia. Wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, ila tu kwa kusema Mola Wetu ni Mwenyezi Mungu.....” (Qur’an 22:39-40).**

Kwa wale watu ambao wametolewa nje ya majumba yao na ardhi zao kwa dhulma na uonevu bila ya kosa lolote lile isipokuwa tu kwamba wamesema: **”Mmiliki Wetu, Mtawala Wetu, Bwana Wetu, Mhifadhi Wetu na Mola Wetu ni Mwenyezi Mungu.”** Mwenyezi Mungu anatoa idhini ya Jihadi. Kosa lao ni kwamba walisema: ”Rabbunallah” yaani, ”Mwenyezi Mungu ndiye Mola Wetu.” Kwa watu kama hao basi Mwenyezi Mungu anatoa idhini ya kupigana.

Angalia ni kwa kiasi gani aya hii inachukua mwelekeo wa sura ya ulinzi. Kisha inaelezea sababu nzima na kamili nyuma ya Jihadi hiyo. Qur’ani inastaajabisha namna inavyofunua na kufichua uhalisia wa mambo na kuyaingiza akilini maelezo yake yote. Kwani hapa inakuja aya maalum kana kwamba tu Qur’ani imekabiliwa na masuala na matatizo yote yanayoibuliwa na Wakristo wa leo, ambao wanasema:

> ”Ewe Qur’ani. Wewe unatarajiwa kuwa ni kitabu kitukufu, unatarajiwa kuwa ni kitabu cha kidini, ni vipi unaweza kutoa idhini ya kupigana? Vita ni jambo baya, siku zote hubiri, sema ’amani’! Sema ’ Utakaso’! Zungumzia ’Ibada’!

Lakini Qur’ani inatuambia: Hapana. Kama upande mwingine unakuwa mchokozi dhidi yetu nasi tusipojitetea, basi tutakabiliwa na machafuko kamili. Nyumba zote za ibada zitabomolewa.:

.....وَلَوۡلَا دَفۡعُ ٱللَّهِ ٱلنَّاسَ بَعۡضَهُم بِبَعۡضٍ لَّهُدِّمَتۡ صَوَٰمِعُ وَبِيَعٌ وَصَلَوَٰتٌ وَمَسَٰجِدُ يُذۡكَرُ فِيهَا ٱسۡمُ ٱللَّهِ كَثِيرًا

**”.....Na lau Mwenyezi Mungu asingeliwakinga watu kwa watu, basi yangelivunjwa mahekalu na makanisa na (sehemu) za kuswalia na misikiti ambayo ndani yake hutajwa jina la Mwenyezi Mungu kwa wingi.....” (22:40)**

Mwenyezi Mungu hakuzuia uchokozi wa baadhi ya watu kwa njia ya wengine, nyumba zote za ibada za dini na madhehebu yote zingebomolewa. Makanisa ya Wakristo, masinagogi ya Mayahudi, mahekalu, Misikiti, sehemu za kusujudia za Waislamu, zote hizi zisingekuwepo tena. Baadhi ya watu wangetenda uchokozi kama huu kiasi kwamba hakuna ambaye angepata uhuru ambao kwawo angemuabudu Mwenyezi Mungu.

وَلَيَنصُرَنَّ ٱللَّهُ مَن يَنصُرُهُۥٓۚ إِنَّ ٱللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ

**“.....Na hakika Mwenyezi Mungu humnusuru yule anayemnusuru Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye enzi.” (22:40)**

Kisha Qur’ani inatoa ahadi ya msaada: **”Mwenyezi Mungu atamnusuru yule anayemnusuru Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye enzi.”** Yeyote anayemnusuru Mwenyezi Mungu, kwa maana ya kwamba, yeyete anayeinusuru

haki na kweli, basi atanusuriwa na Mwenyezi Mungu, Naye ni Mwenye nguvu na daima Ndiye Mshindi.

Sasa angalia namna jinsi Mwenyezi Mungu anavyowaelezea wale anaowanusuru. Mwenyezi Mungu anawanusuru watu wanaojilinda wenyewe, watu ambao, pindi wanapoanzisha serikali, wanaunda moja ya mistari hii:

ٱلَّذِينَ إِن مَّكَّنَّٰهُمۡ فِي ٱلۡأَرۡضِ

**"Wale ambao tukiwamakinisha katika ardhi ....." (22:41),**

watu ambao pindi Mwenyezi Mungu anapowapatia sehemu ya makazi yao na wakaanzisha serikali yao, watu ambao, Mwenyezi Mungu anapowapa nguvu na mamlaka, huwa wanaunda dola juu ya aya au mistari hii. Mistari gani?

" أَقَامُواْ ٱلصَّلَوٰةَ

**"....husimamisha swala....."**

Wanaanzisha ibada ya Mwenyezi Mungu.

وَءَاتَوُاْ ٱلزَّكَوٰةَ

**".....na wakatoa Zaka"**

Swala ndio fungamano sahihi la kiroho baina ya mwanadamu na Mwenyezi Mungu, na Zaka ndio fungamano sahihi la kiroho la ushirikiano baina ya watu mmoja mmoja. Watu wanaomwabudu Mwenyezi Mungu kwa uaminifu kamili na kusaidiana wenyewe kwa wenyewe.

وَأَمَرُواْ بِٱلْمَعْرُوفِ وَنَهَوْاْ عَنِ ٱلْمُنكَرِ

**“.....na wakaamrisha mema na kukataza mabaya.”**

Wanajichukulia wenyewe wajibu wa kuendeleza yaliyo mema na kupigana na yaliyo mabaya.

وَلِلَّهِ عَـٰقِبَةُ ٱلْأُمُورِ

**“.....na kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo ya mambo yote.”**

Matokeo ya mambo yote, masuala yote yapo ”Mikononi” mwa Mwenyezi Mungu.

Tulichojifunza mpaka kufikia hapa ni kwamba Qur’ani kimsingi imeielezea na kuichanganua jihadi kama sio vita vya uchokozi au vya ubora au vya madaraka., bali ni upinzani dhidi ya uchokozi na uvamizi.

Bila shaka aina za uchokozi ambazo ni za kupingwa haziko siku zote kama mwelekeo wa kundi moja kuvamia nchi ya jingine. Pengine huenda aina ya uchokozi itakuwa ni ya mwelekeo wa upande mwingine katika nchi yao wenyewe kutesa na kukandamiza kikundi kutoka miongoni mwao wenyewe, kikundi ambacho ni dhaifu na

kisicho na uwezo, ambao kwa lugha ya Qur'ani wanaitwa *mustadhafin*. Katika hali kama hiyo, Waislam hawawezi kupuuza na kukaa mbali. Waislam wana wajibu wa kuwakomboa watu wanaoteswa kama hao. Au pengine huo upande mwingine utasababisha hali mbaya ya ukandamizaji kiasi kwamba wito wa haki, wito wa ukweli, upendo na uadilifu hautaruhusiwa kushamiri; watakuwa wameweka mpaka na kipingamizi ambacho ni lazima kivunjwe. Zote hizi ni aina za uchokozi. Waislamu ni lazima wawakomboe wanadamu kutoka kwenye minyororo ya ufungwaji wa mawazo na vifungo vinginevyo. Katika hali zote hizi jihadi ni hitajio la muhimu kabisa; na jihadi kama hiyo ni katika ulinzi, katika upinzani dhidi ya dhulma, dhidi ya uonevu na ukandamizaji, na dhidi ya uchokozi.

Neno 'ulinzi' katika maana yake ya kawaida linamaanisha upinzani dhidi ya dhulma iliyokuwepo au ukosefu wa haki na uonevu, lakini aina za dhulma na aina za uchokozi ambazo jihadi dhidi yao, kwa maoni ya Uislamu ni muhimu kabisa, bado ni za kujadiliwa.

# MLANGO WA PILI

## NI ULINZI AU UCHOKOZI

### VIPINGAMIZI VYA UKRISTO KWENYE UISLAM:

Awali tumesema kwamba moja ya nukta ambayo, katika maoni yake yenyewe, ulimwengu wa ki-Kristo unaiona kama ni kipengele dhaifu cha Uislamu ni suala la Jihadi ya Kiislamu, ambayo unaushawishi useme kwamba Uislamu ni dini ya vita, sio dini ya amani, ambapo Ukristo ni dini ya amani. Unasema kwamba vita ni mbaya moja kwa moja na amani ni nzuri, na kwamba dini yoyote iliyoundwa kimungu ni lazima itetee amani ambayo ndio nzuri. Hadi jana Ukristo umeyaangalia mambo kwa mtazamo wa tabia njema, tabia njema kwa Ukristo pekee; tabia njema ambayo imefikia hatua ya 'kugeuza shavu la pili' tabia njema ambayo inalea uweupe tupu. Lakini Ukristo leo umebadilisha nafasi. Umebadilisha sura yake. Sasa unaangalia mambo kutoka kwenye mwelekeo mwingine, na unaendesha propaganda yake kupitia kwenye njia tofauti, kupitia njia ya haki za msingi za binadamu, na haki ya msingi ya binadamu kwenye uhuru. Kupitia njia ya **"vita kuwa vinapingana kabisa na haki ya uhuru."** Kupitia uhuru wa imani, uhuru wa hiari, uhuru wa kuchagua dini, utaifa na mambo mengine. Lakini Uislamu unaliangalia jambo hilo kutoka kwenye mitazamo yote, kutoka kwenye mtazamo wa kimaadili na viwango vya uadilifu, na pia kutoka kwenye mtazamo wa haki za binadamu na maadili 'mapya' ya kibin-

adamu. Nilielezea jibu la jambo hili katika mlango uliotangulia. Ni dhahiri na wazi kabisa kwamba kile wanachokisema Wakristo sio sahihi hata kidogo.

Bila shaka amani ni nzuri. Hakuna shaka kuhusu hilo. Na vita, kwa ajili ya uchokozi dhidi ya watu wengine, watu ambao hawana nia yoyote dhidi ya mchokozi, hawana makusudio yoyote dhidi ya jamii hiyo yenye uchokozi , vita kwa ajili ya kukalia ardhi ya taifa jingine na ya kupora mali zake, kwa ajili ya kuwatumikisha raia wake, kwa ajili ya kuwatiisha kwenye ushawishi na kwenye sheria za mvamizi huyo, hivyo, bila shaka ni vita vibaya. Uvamizi na uchokozi ni mambo mabaya. Lakini vita vyote, katika pande zote, sio kwamba siku zote ni ya uchokozi. Vita vinaweza kuwa vya uchokozi na vinaweza pia kuwa ni vya kujibu uchokozi, kwani wakati mwingine majibu ya uchokozi ni lazima yatolewe kwa nguvu. Kuna nyakati nyingine nguvu hiyo inakuwa ndio jibu pekee ambalo linaweza kutolewa.

Dini yoyote ile, kama ni iliyokamilika, ni lazima iwe na maelekezo juu ya uchokozi juu yake yenyewe na kwa mataifa mengine kadhalika. Ni kwa ajili ya tukio kama hilo ambapo dini lazima iwe na sheria juu ya vita, sheria ya jihadi. Wakristo wanasema kwamba amani ni nzuri, nasi tunalikubali hilo; kweli amani ni nzuri. Lakini ni vipi kuhusu kutiishwa (kusalimu amri), kudhalilishwa na mateso? Na haya nayo pia ni mazuri, kutiishwa, kudhalilishwa na kuteswa? Kama mamlaka moja inakabiliwa na mamlaka nyingine, na zote zinatetea amani, zote zinapenda, kwa lugha ya kisasa, kuishi maisha ya pamoja ya amani, bila ya mojawapo kutamani kuivamia nyingine, zote zikawa zinahiari kuishi kwa amani pamoja na kuheshimiana, basi hii ndio inaitwa amani na ni nzuri na ya msingi na muhimu.

Kuna wakati hata hivyo, kundi moja linakuwa ni chokozi, na kwa kisingizio cha kwamba vita ni mbaya, ule upande mwengine unakubali

kusalimu amri, huu ni udhalilishaji na sio amani. Huku ni kuhiari kukubali kudhalilishwa na mateso. Utii kama huo mbele ya mabavu, kamwe hauwezi kuitwa ni amani. Kwa mfano, wakati unapokuwa unapita jangwani, haramia mwenye silaha anakushambulia ghafla na anakuamrisha: 'Toka kwenye gari yako upesi, mikono juu na toa chochote kile ulichonacho.' Hapa unajisalimisha mwenyewe na kumwambia: 'Mimi ni mtetezi wa amani na ninapingana na vita moja kwa moja. Nitakubali kila utakachoniamuru. Nakupa pesa zangu, mizigo na vifurushi vyangu, gari yangu na nitatii kila utakachosema. Wewe sema lolote unalotaka nami nitakupatia. Kwa sababu mimi natetea amani.' Huu sio utetezi wa amani. Huku ni kukubali kudhalilishwa. Katika hali hii, mtu lazima ajitetee na kujilinda mwenyewe, mali yake na heshima yake, isipokuwa kama anajua kwamba kama akiamua kujitetea, mali yake itaporwa, damu yake itamwagika na hakutakuwa na maana yoyote ndani yake. Kwa kweli ni lazima izingatiwe akili kwamba wakati mwingine kwamba kutoa mhanga damu yake mtu ni jambo lenye athari na nguvu sana, lakini pale inapokuwa damu ya mtu itamwagika na kila kitu kikafika mwisho, kufanya upinzani sio busara wala hekima na mtu lazima akubali kutoa muhanga pesa na mali yake ili kuokoa maisha yake.

Kuna tofauti kati ya utetezi wa amani na kukubali udhalilishwaji. Uislamu kamwe hauruhusu kukubali kudhalilishwa, ambapo wakati huo huo unatetea amani kwa nguvu zote. Ninachotaka kusisitiza hapa ni umuhimu wa hili jambo ambalo Wakristo na wengineo wamekuwa wakiushambulia na kuupinga Uislamu, wakidai kwamba ni kipengele dhaifu cha Uislam. Wao wanadai kwamba, kwa mujibu wa mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Uislamu ni dini ya upanga; Waislamu walinyanyua panga zao juu ya vichwa vya watu na kusema: **'Chagua kuwa Mwislamu au kufa,'** na kwamba watu wakaukubali Uislamu ili wabakia hai. Kwa hiyo, nadhani ni muhimu

kwetu sisi kulichambua jambo hili kinagaubaga na kwa uangalifu sana, na tutatumia sio tu aya za Qur'ani, bali pia hadith za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zilizothibitika na kutupia macho kidogo kwenye maisha yake. Tutaanza na aya za Qur'ani.

## AYA ZENYE AMRI KAMILI JUU YA JIHADI

Nilisema kwamba baadhi ya maagizo ya Qur'ani kuhusu jihadi dhidi ya wasioamini (makafiri) zina amri kamili isiyo na sharti, ambapo ina maana kwamba zinaeleza hivi tu: **"Ewe Mtume, pigana na makafiri na washirikina."** Kwa mujibu wa aya fulani, baada ya muda ambao umetolewa kwa washirikina (miezi minne), kama hawakukubali Uislam au hawakuhama, basi hao ni wa kuuliwa. (Je, hii inarejelea kwenye viunga vya Makka na kuzunguka lile eneo takatifu, au ni kwa kila mahali? Swali hili lazima lijadiliwe baadaye). Aya ambayo tunaanza nayo mjadala wetu pia ni kuhusu Watu wa Kitabu:

قَٰتِلُواْ ٱلَّذِينَ لَا يُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ وَلَا بِٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِ وَلَا يُحَرِّمُونَ مَا حَرَّمَ ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥ وَلَا يَدِينُونَ دِينَ ٱلۡحَقِّ مِنَ ٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلۡكِتَٰبَ حَتَّىٰ يُعۡطُواْ ٱلۡجِزۡيَةَ عَن يَدٖ وَهُمۡ صَٰغِرُونَ ﴿٢٩﴾

**"Piganeni na wale wasiomwamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho, wala hawaharamishi aliyoharamisha Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, wala hawashiki dini ya haki, miongoni mwa waliopewa Kitabu, mpaka watoe kodi kwa mkono hali wametii." (Qur'an 9:29)**

Aya ifuatayo vile vile ni kuhusu jambo hilo hilo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِيُّ جَٰهِدِ ٱلۡكُفَّارَ وَٱلۡمُنَٰفِقِينَ .....

**"Ewe Mtume! Pambana na makafiri na wanafiki....." (Qur'an 9:73)**

Kama tungekuwa tuzingatie kwenye aya hii tu, tungesema kwamba Uislamu kwa ukamilifu kabisa unawaagiza Waislamu kupambana na makafiri na wanafiki na kwamba Waislamu hao kamwe wasije kuwa na hali ya amani nao na wawapige, kwa nguvu kabisa kiasi wawezavyo. Kama tukitafsiri aya hizo hapo juu kwa namna hii, basi tutakuja kuamini kwamba Qur'ani inatuagiza sisi kupambana bila masharti na wale wasiokuwa Waislamu.

Nimeeleza hata hivyo, kwamba kuna kanuni ya kiwanachuoni inayoonyesha kwamba, wakati aya zote, yenye amri kamili isiyo na sharti na ya amri yenye masharti zinapokuwepo pamoja, yaani, kama kuna maagizo kwamba mahali pamoja ni amri kamili isiyo na sharti lakini mahali pengine ni amri iliyoambatana na sharti, basi kwa mujibu wa Maulamaa, ile ya amri kamili isiyo na sharti lazima itafsiriwe kama yenye masharti. Aya ambazo nimezitaja hivi punde ni zenye amri kamili isiyo na sharti. Kuna aya zingine kuhusu jambo hilo hilo ambazo ni zenye masharti:

**'Enyi Waislamu piganeni na hao washirikina kwa sababu wamo kwenye uchokozi dhidi yenu, kwa sababu wamo kwenye hali ya kivita pamoja nanyi, na kwa hiyo ni dhahiri kwamba mnapaswa kupigana dhidi yao"**

Kwa hiyo inakuwa wazi kwamba pale Qur'ani inaposema: 'Ewe Mtume! Pambana dhidi ya makafiri na wanafiki,' ina maana kwamba

ni lazima tupigane na hao makafiri na wanafiki ambao wanatupiga sisi na ambao wataendelea kupigana kama tukiwapiga.

## AYA ZENYE MASHARTI

Qur'ani Tukufu inasema:

وَقَٰتِلُوا۟ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ ٱلَّذِينَ يُقَٰتِلُونَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوٓا۟ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ
لَا يُحِبُّ ٱلْمُعْتَدِينَ

**"Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaowapiga, wala msichokoze. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wachokozi."**
**(Qur'an 2:190)**

Enyi mlioamini, piganeni na wale wanaowapiga, yaani piganeni nao kwa sababu wanawapigeni, lakini msipituke mipaka. Je, haina maana kwamba tusiwe wavamizi? Ni dhahiri inawazungumzia wale wanaotupiga na kwamba sisi tusipigane na mwingine yoyote yule, na kwamba ni katika uwanja wa mapambano tu ambao tunapaswa kupigana humo. Tunapaswa kupigana na kundi maalum la watu, yaani wale askari ambao upande wa pili umewatuma, wanaume wa vita, wamejiandaa kupigana dhidi yetu sisi na ambao kwa hakika wanatupiga. Lakini usipituke mipaka wakati mnapopigana nao. Hii ina maana gani? Ina maana kwamba piganeni na watu tu wanaokupigeni, piganeni na askari wao katika uwanja wa mapambano. Piganeni na wale askari ambao wametumwa kuja kupigana. Medani ya vita sio mahali pa furaha, ni uwanja wa kupambanisha panga, kurushiana

risasi na kupigana. Bali haturuhusiwi kuwasumbua raia bila sababu, wanaume, wanawake na watoto. Hamruhusiwi kufanya ukatili ambao ni sawa na uvamizi kama vile kukata miti, kufunika mifereji yao na kadhalika.

Hata hivyo, katika baadhi ya hali, tunapaswa kubomoa nyumba ili kusafisha njia kwa ajili ya vita, hili ni jambo jingine. Lakini kama kubomoa nyumba sio sehemu ya oparesheni ya kijeshi, hilo haliruhusiwi katika Uislamu.

Aya nyingine yenye masharti, ya kwanza kushushwa juu ya jihadi, inasema kwamba kwa sababu ule upande mwingine umechomoa panga zao dhidi yetu, basi nasi tunaweza kufanya kama vivyo. Na katika aya nyingine ya Surat-Tawba tunaambiwa hivi:

..... وَقَٰتِلُوا۟ ٱلْمُشْرِكِينَ كَآفَّةً كَمَا يُقَٰتِلُونَكُمْ كَآفَّةً

**“.....Na piganeni na washirikina nyote, kama wanavyopigana nanyi wote.....” (Qur’an 9:36)**

## KUKIMBILIA KUWALINDA WANAOONEWA

Kabla ya kuigusa mada hii na aya zinazohusiana nayo, jambo moja lazima lisemwe hapa. Nilieleza kwamba ruhusa kwa ajili ya jihadi inapaswa kuwa na masharti fulani. Masharti gani? Moja ni kwamba ule upande pinzani upo katika hali ya uchokozi. Wanatushambulia sisi, na kwa sababu wanapigana dhidi yetu ni lazima tupigane nao. Je masharti ya jihadi yanaishia kwenye hili tu peke yake: kwamba ule upande mwingine unataka kutupiga sisi? Au kuna vipengele ving-

ine? Wakati upande huo mwingine una hatia ya udhalimu wa dhahiri juu ya kundi jingine la wanadamu, na tunao uwezo wa kuwaokoa binadamu hao kutoka kwenye makucha ya huyo mchokozi, kama hatutawaokoa, basi tutakuwa tunamsaidia huyo mchokozi dhidi ya hao wanaoonewa. Kama kundi hilo ni la Waislamu , kama vile Wapalestina wa leo ambao wamefukuzwa kutoka kwenye majumba yao, mali zao zimeporwa, na wamekumbwa na aina zote za uvamizi, wakati huo huo, sasa hivi mvamizi huyo hana dhamira yoyote dhidi yetu sisi. Je, inaruhusiwa kwetu sisi katika mazingira kama hayo kukimbilia kwenda kuwasaidia wale Waislamu wanaokandamizwa ili kuwakomboa?

Sio tu kwamba inaruhusiwa, bali kwa kweli ni wajibu. Haitakuwa ni suala la kuanzisha hasama, itakuwa ni kukimbilia kwenye utetezi wa wale wanaokandamizwa, hususan kama ni Waislamu, ili kuwagomboa kwenye makucha ya udhalimu.

Lakini kama yule mtu au kundi linalokandamizwa sio la Waislam, basi huyo dhalimu anaweza kuwa wa namna mbili. Kuna wakati ambapo dhalimu amewaweka watu kwenye ombwe na kuzuia wito wa Uislamu. Uislamu unajipa wenyewe haki ya kueneza ujumbe wake kote duniani, lakini inategemea juu ya kuwepo kwa uhuru juu ya kuenea kwake.

Hebu fikiria serikali fulani ambayo inawaambia Waislam ambao wanatoa wito wa Uislamu kwenye taifa: ‘Hamna haki ya kusema hayo mnayoyasema. Sisi hatuliruhusu hilo.’ Katika hali kama hizi, hairuhusiwi sisi kupigana na taifa hilo, na watu ambao hawana lawama na wasiojua kitu. Lakini je, inaruhusiwa sisi kupigana dhidi ya huo utawala dhalimu ambao unajiegemeza wenyewe kwenye itikadi chafu iliyooza ambayo unaitumia kama mnyororo kwenye shingo za watu kuwafunga katika uchochoro wa giza na kuwatenga na wito wa haki? Je, tunaruhusiwa kupigana na utawala huo ili

kuondoa kikwazo hicho? Au katika hali halisi, inaruhusiwa sisi kupigana dhidi ya jela hiyo ya ukandamizaji? Katika Uislamu hili pia linaruhusiwa, kwani hili kwa lenyewe litakuwa kama ni namna ya upinzani dhidi ya dhulma, dhidi ya kunyimwa haki na kuonewa. Inaweza kuwa kwamba wale wanaokosewa, wanaokandamizwa hawaitambui hali ya dhulma hiyo na hawajatafuta msaada, lakini kwa kweli hakuna haja wa wao kuuomba msaada huo.

Huko kutafuta au kuomba msaada ni jambo jingine, tukichukulia kwamba wale wanaoonewa wanatafuta msaada kutoka kwetu, je inaruhusiwa au ni wajibu kwetu sisi kuwasaidia hao? Hata kama hawakuomba msaada, je bado inaruhusiwa sisi kuwasaidia? Jawabu ni kwamba sio lazima wao waombe msaada wetu. Ule ukweli mwepesi kwamba wanaoonewa wanakandamizwa, kwamba utawala dhalimu umejenga ukuta, umeweka kizuizi, kwa ajili ya faida yake wenyewe, kuuzuia umma usiutambue ule wito ambamo mna ustawi na furaha kwa ajili ya umma huo, wito ambao kama wakiusikia na wakautambua, wana uhakika wa kuukubali, unausukuma Uislamu kusema kwamba tunaweza kukivunja kikwazo hicho ambacho kipo kwa sura ya serikali kandamizi, baina yake na watu hao.

## VITA VYA MWANZONI MWA UISLAMU

Vita vingi vya mwanzoni mwa Uislamu vilipiganwa kwa ajili ya kuondoa vikwazo vilivyokuwa katika njia ya kueneza ujumbe wake wa Uislamu. Waislamu ambao walikwenda vitani walikuwa wakisema kwamba wao hawana ugomvi na watu wa ulimwengu, na kwamba walikuwa wakipigana na serikali ili kuwaokoa watu kutokana na dhiki na utumwa uliopandikizwa juu yao na serikali hizo. Wakati Rustam Farrukhzad, mtawala bingwa wa kabla ya Uislamu

huko Uajemi aliwauliza Waislamu ni nini lilikuwa lengo lao, wao wakamjibu:

> 'Kuwafanya watu wamuabudu Mwenyezi Mungu badala ya kumuangukia mwanadamu. Lengo letu ni kuwakomboa viumbe hawa wa Mwenyezi Mungu, ambao kwa hila na ukatili, wewe umewaweka kwenye kongwa ya utumwa na kuwafunga kwa utiifu kwenu wenyewe. Sisi tutawatoa kwenye kongwa hiyo ya utumwa kwenu. Tutawafanya wawe huru, tutawafanya wawe watiifu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, wawe wafuasi wa Muumba Wao, sio wafuasi wa kilichoumbwa na Yeye kama vile tu mlivyo ninyi.'

Katika barua ambazo Mtukufu Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) alizowaandikia Watu wa Kitabu, yeye hususan alikuwa akiingiza na aya hii ya Qur'ani:

قُلْ يَٰٓأَهْلَ ٱلْكِتَٰبِ تَعَالَوْا۟ إِلَىٰ كَلِمَةٍ سَوَآءٍۭ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا ٱللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِۦ شَيْـًٔا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّن دُونِ ٱللَّهِ ۚ .....

**'Sema: Enyi watu wa Kitabu! Njooni kwenye neno la usawa baina yetu na baina yenu. Kwamba tusimwabudu yoyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote; wala baadhi yetu wasiwafanye baadhi kuwa waungu zaidi ya Mwenyezi Mungu..... (3:64).**

Aya hii ilimuagiza Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuwalingania watu wa Kitabu (watu wale wale ambao kuhusu wao maagizo ya jihadi yalishushwa) wakubali neno maalum, neno ambalo lilikuwa ni hilo hilo kuwahusu wao kama lilivyokuwa kuhusu sisi. Haisemi kwamba wanapaswa kukubali neno ambalo ni kwa manufaa yetu sisi na lililohusishwa kwetu sisi tu. Inasema kwamba wao wanapaswa kukubali neno ambalo ni hilo hilo kwa wote.

Kama kwa mfano, tukiwaambia watu: ’Njooni enyi watu, kubalini lugha yetu,’ hapo watu hao wanayo haki ya kusema: ’Kwa nini? Sisi wenyewe tunayo lugha yetu, kwa nini tukubali lugha yenu ninyi?’ Ama tunaweza kusema: ’Njooni na mkubali tabia na desturi zetu maalum.’ Wao wanaweza wakasema: ‘Kwa nini tukubaliane na tabia na desturi zenu? Sisi tunazo za kwetu wenyewe.’ Lakini kama tukisema: Njoni mkubaliane na jambo hili ambalo sio la kwetu na sio lenu bali ni la kila mtu; Mwenyezi Mungu ni Mungu wetu sote, kwa hiyo mkubalini Yeye,’ hili halihusiani tena na sisi tu. Wakati tunaposema: ‘Mwabuduni Yeye ambaye ni Muumba wetu sisi na Muumba wenu ninyi, bali Yeye ambaye ni Muumba wa kila kitu,’ hapo hili ni lile lile kwao kama lilivyo kwetu sisi. Qur’ani inasema:

تَعَالَوۡاْ إِلَىٰ كَلِمَةٖ سَوَآءِۭ بَيۡنَنَا وَبَيۡنَكُمۡ

**‘.....Njooni kwenye neno la usawa baina yetu na baina yenu.....’**

ni Mwenyezi Mungu, Muumba wetu sisi sote Ndiye wa kuabudiwa. Na kauli nyingine ambayo ni yenye manufaa makubwa sana kwetu na kwao pia ni:

وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّن دُونِ ٱللَّهِ

**'.....wala baadhi yetu wasiwafanye baadhi kuwa waungu zaidi ya Mwenyezi Mungu.....'**

Hii ina maana kwamba ile hali ya utaratibu wa kijamii wa bwana na mtwana umefutwa, na utaratibu wa usawa baina ya binadamu umesimikwa. Aya hii inadhihirisha kwamba, kama tukipigana, tunapigana kwa ajili ya kile ambacho ni kile kile cha sawa kuhusu binadamu wote. Baada ya kulieleza hili, sasa tunaweza kusema kwamba mojawapo ya masharti ambayo aya yenye amri kamili inaweza kupewa ni kwamba, endapo kundi la watu limetwishwa uonevu wa kundi fulani, inakuwa inaruhusiwa kwetu sisi kupigana ili kulikomboa lile kundi linaloonewa.

Sasa kuna aya nyingine mbili ambazo ninapenda kuzisema, ya kwanza yake ikiwa ni ile aya kutoka kwenye Surat al-Anfal:

وَقَـٰتِلُوهُمۡ حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتۡنَةٌ وَيَكُونَ ٱلدِّينُ كُلُّهُۥ لِلَّهِ

**'Na piganeni nao mpaka kusiwe na fitna na dini yote iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.....' (8:39).**

Hii ina maana gani? Ina maana kwamba tunapaswa kupigana na wale wanaosababisha fitna na machafuko miongoni mwetu na ambao wanataka kutufanya sisi Waislamu tuiachilie mbali dini yetu. Kwa watu kama hawa, tunapaswa kupigana mpaka ile fitina wanayosababisha itoweke. Hili peke yake ni sharti. Na sharti la ziada limo kwenye aya ya 75 kutoka Suratun-Nisa:

وَمَا لَكُمْ لَا تُقَـٰتِلُونَ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱلْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ
ٱلرِّجَالِ وَٱلنِّسَآءِ وَٱلْوِلْدَٰنِ ...

**'Na mna nini hampigani katika njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanaoonewa katika wanaume na wanawake na watoto.....' (4:75).**

Enyi Waislamu, kwa nini hampigani katika njia ya Mwenyezi Mungu na njia ya wale ambao hawana msaada? Wanaume, wanawake na watoto ambao hawana msaada katika mateso; kwa nini hampigani kwa ajili yao? Kwa nini hampigani ili kuwaokoa hao?

## KUTAFSIRI AYA ZISIZO NA SHARTI KAMA ZENYE MASHARTI

Hizi aya tano ambazo tumezizungumzia zimeonyesha kwamba, kama maagizo ya Uislamu juu ya jihadi yaliyotolewa katika baadhi ya sehemu ni ya amri kamili isiyo na sharti, na mahali pengine ni yenye masharti, basi yale ya amri kamili isiyo na sharti lazima yatafsiriwe na wanachuoni kama yale yenye masharti.

## HAKUNA KULAZIMISHANA KATIKA DINI

Ndani ya Qur'ani tuna kundi la aya ambazo zinaeleza bayana kwamba dini ni jambo la kukubaliwa kwa hiari kabisa na haiwezi kulazimishwa juu ya mtu, na hili linathibitisha kile tulichokuwa tukikisema, kwamba katika Uislamu hakuna mtu yeyote anayeweza

kulazimishwa, aambiwe kwamba ama kuwa Mwislamu au kufa. Aya hizi zinafafanua zile aya zenye amri kamili kwa njia tofauti.

Mojawapo ni ile sehemu ya ’Ayat-ul-Kursi’ (2:255-257) nayo inafahamika vema sana, nayo ni:

لَآ إِكۡرَاهَ فِي ٱلدِّينِۖ قَد تَّبَيَّنَ ٱلرُّشۡدُ مِنَ ٱلۡغَيِّ

**“Hakuna kulazimisha katika dini; uongofu umekwisha pambanukana upotofu.....” (Qur’an 2:256).**

Ambayo ina maana kwamba ni lazima tuielezee kwa uwazi kabisa ile njia ya haki kwa watu. Hakuna nafasi ya matumizi ya nguvu katika dini, mtu yeyote asilazimishwe kuikubali dini ya Uislamu. Aya hii iko dhahiri kabisa katika maana yake. Katika tafsiri za Qur’ani imeandikwa kwamba Ansari mmoja ambaye mwanzoni alikuwa mshirikina alikuwa na watoto wawili wa kiume ambao walikuwa wameingia katika Ukristo. Vijana wawili hawa walikuwa wamependezwa sana na Ukristo na walikuwa wamejitolea sana kwao, lakini baba yao sasa alikuwa keshasilimu ni Mwislam na alikuwa ameghadhibika kwamba watoto wake wamekuwa Wakristo. Alikwenda kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akamwambia: ”Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Niwafanyeje hawa watoto wangu ambao wamekuwa Wakristo. Hawaukubali Uislamu. Je, unanipa ruhusa ya kuwalazimisha kuacha dini yao hiyo na kuwa Waislamu?” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: ”Hapana. Hakuna kulazimisha katika dini.”

Kuhusu mazingira ambamo aya hii imeshuka, imeandikwa kwamba kuna makabila mawili, la Aws na Khazraj, ambayo yalikuwa yanaishi Madina, na vilevile walikuwa ndio wakazi wa asili wa

Madina. Mwanzoni mwa kufika Uislamu, wao walikuwa wanaishi humo pamoja na makabila makubwa kadhaa ya Wayahudi ambao walikuja Madina katika kipindi cha baadaye. Mojawapo lilikuwa kabila la Bani Nadhir, na jingine lilikuwa la Bani Quraidhah, ambapo kulikuwa bado na kabila jingine kubwa la Wayahudi ambalo liliishi pembezoni mwa mji huo.

Wayahudi hao, wakiwa na Uyuda (*Judaism*) kama dini yao na wakiwa pia na kitabu kitakatifu, wakaja wakaonekana kama ndio watu waliokuwa na elimu katika jamii hiyo, ambapo miongoni mwa wakazi wa asili wa Madina, ambao walikuwa washirikina na kwa jumla wasio na elimu, kulikuwa kumejitokeza upya kikundi kidogo pia cha watu waliokuwa na uwezo wa kuandika na kusoma. Hao Wayahudi, kama matokeo ya utamaduni wao wa juu na ueneaji mpana wa mawazo yao, walifanya ushawishi mkubwa juu ya kundi hili. Hivyo, licha ya ukweli kwamba dini ya hao Aws na Khazraj ilikuwa tofauti kabisa na hiyo ya Wayahudi, hata hivyo waliruhusu wenyewe kuathirika na maoni ya Wayahudi. Matokeo yake, walikuwa wakati mwingine wakiwapeleka watoto wao kwa hao Wayahudi kwenda kupata elimu, na wakati walipokuwa miongoni mwa hao Wayahudi, watoto hao walikuwa wakati mwingine wakiikana dini yao ya kipagani ya ushirikina na wakajiunga kwenye dini ya Uyuda.

Hivyo, wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipoingia Madina, kundi la vijana hawa kutoka kwenye mji huo walikuwa wakifundishwa na Wayahudi na walikuwa wenyewe wamejichagulia hiyo dini ya Wayahudi ambayo baadhi yao walichagua kutoikana. Wazazi wa watoto hawa waliingia katika Uislamu, lakini bado watoto wao hawakuiacha dini yao mpya, Uyuda. Na pale ilipoamuliwa kwamba Wayahudi wanapaswa waondoke Madina (kama adhabu kwa ajili ya fujo ambayo walikuwa wameichochea) watoto wale pia nao waliondoka pamoja na wenzao wa Kiyahudi. Wazazi wao

walikwenda kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wakimuomba ruhusa ya kuwatenganisha watoto wao na Wayahudi hao, kuwalazimisha kuachana na dini ya Wayahudi na kuwa Waislamu, ruhusa ambayo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuwapatia. Wao wakasema: ”Ewe Mtume! Turuhusu kuwalazimisha kuachana na dini yao hiyo na kuingia kwenye Uislamu.” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwaambia: ”La hasha. Kwa vile sasa wamechagua kwenda na hao Wayahudi, waacheni waende pamoja nao.” Na wafasiri wanasema kwamba ilikuwa ni hapo ambapo ndipo kwamba aya hii: **”Hakuna kulazimisha katika dini; uongofu umekwisha pambanuka na upotofu.....” (2:256)** ikashuka.

Aya nyingine maarufu ni hii:

ٱدۡعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلۡحِكۡمَةِ وَٱلۡمَوۡعِظَةِ ٱلۡحَسَنَةِۖ

**“Waite kwenye njia ya Mola Wako kwa hekima na mawaidha mazuri.....” (Qur’an 16:125)**

Walinganie watu kwenye njia ya Mola Wako. Vipi? Kwa kutumia nguvu na upanga? Hapana! Kwa maonyo mazuri na ushauri.

وَجَٰدِلۡهُم بِٱلَّتِي هِيَ أَحۡسَنُ

**“.....Na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora.....” (Qur’an 16:125)**

Na wale wanaojadiliana nasi, ni lazima pia tujadiliane nao kwa namna iliyo bora kabisa. Aya hii imetambulisha wazi kabisa njia kwa ajili ya Waislamu kupeleka ujumbe kwa watu.

Katika aya nyingine tunaambiwa kwamba:

وَقُلِ ٱلْحَقُّ مِن رَّبِّكُمْ ۖ فَمَن شَآءَ فَلْيُؤْمِن وَمَن شَآءَ فَلْيَكْفُرْ ۚ

**"Sema hii ni kweli itokayo kwa Mola Wenu, basi atakaye aamini, na atakaye akufuru....." (Qur'an 18:29)**

Yeyote yule anayetaka kuamini basi ataamini, na yeyote anayetaka kukanusha basi atakanusha. Kwa hiyo aya hii vilevile imeeleza kwamba imani na kufuru vinaweza tu kuchaguliwa na mtu mwenyewe, haviwezi kulazimishwa na mmoja juu ya mwingine. Hivyo Uislamu hausemi kwamba wengine sharti walazimishwe kusilimu na kuwa Waislamu. Kama watu hawaukubali Uislamu, hawawezi kuwa ni watu wa kuuliwa, uamuzi ni wao. Uislamu unasema kwamba yeyote anayetaka kuamini ataamini, na yeyote anayetaka kukufuru atakufuru. Kuna aya hii vilevile:

وَلَوْ شَآءَ رَبُّكَ لَءَامَنَ مَن فِي ٱلْأَرْضِ كُلُّهُمْ جَمِيعًا ۚ أَفَأَنتَ تُكْرِهُ ٱلنَّاسَ حَتَّىٰ يَكُونُوا۟ مُؤْمِنِينَ ﴿٩٩﴾

**"Lau angelitaka Mola Wako, wangeliamini wote waliomo ardhini. Basi je wewe utawalazimisha watu wawe Waumini?" (10:99)**

Aya hii anaambiwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Yeye (s.a.w.w.) kwa kweli aliwapenda watu na aliwataka wawe waumini wa kweli. Qur'ani inasema kwamba matumizi ya nguvu katika suala la imani

hayana maana. Kama nguvu ingekuwa ni halali, basi Mwenyezi Mungu Mwenyewe, kwa Mamlaka Yake ya uumbaji angewafanya watu wote kuwa ni waumini. Mwenyezi Mungu, pamoja na Mamlaka Yake yote ya uumbaji na ulazimishaji hakuwalazimisha binadamu kuwa waumini wa kweli na amewapa hiari ya kuchagua. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) pia alikuwa anawaacha wao wajichagulie wenyewe. Yule ambaye moyo wake unapenda basi atakuwa muumini mzuri, na yule ambaye moyo wake haupendi kuamini basi hatoamini.

Aya nyingine iliyozungumziwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) inasema:

لَعَلَّكَ بَـٰخِعٌ نَّفْسَكَ أَلَّا يَكُونُوا۟ مُؤْمِنِينَ ﴿٣﴾

**"Huenda ukaangamiza nafsi yako kwa kuwa hawawi waumini." (Qur'an 26:3).**

إِن نَّشَأْ نُنَزِّلْ عَلَيْهِم مِّنَ ٱلسَّمَآءِ ءَايَةً فَظَلَّتْ أَعْنَـٰقُهُمْ لَهَا خَـٰضِعِينَ ﴿٤﴾

**"Tungelipenda tungeliwateremshia kutoka mbinguni ishara zikainyenyekea shingo zao." (26:4).**

'Ewe Mtume! Inakuwa kana kwamba unadhamiria kujiua mwenyewe kwa sababu hawakuamini, kana kwamba unataka kujiangamiza mwenyewe. Usiwe mwenye huzuni kiasi hicho kwa ajili yao. Sisi, pamoja na Mamlaka Yetu ya Uumbaji na Nguvu, kama tungependa kuwalazimisha watu kuamini, tungeweza kufanya hivyo kwa urahisi

sana. Kama tungependa, Sisi tungeishusha mbingu kama ishara ya kunyenyekea shingo zao, ili wao wawe watiifu.' Hapa Mwenyezi Mungu anasema kwamba kama angetaka kushusha kutoka mbinguni ishara, adhabu, na kuwaambia watu kwamba ama wawe waumini wa kweli au waangamizwe na adhabu hiyo, watu wote kwa kulazimishwa wangekuwa waumini, lakini Yeye hafanyi hivyo kwa sababu Yeye anataka watu wajichagulie wenyewe.

Aya hizi zinaendelea zaidi kufafanua lile wazo la Jihadi katika Uislamu na kuweka wazi kwamba jihadi katika Uislamu sio kile baadhi ya makundi yenye upendeleo binafsi yalivyosema. Aya hizi zinafafanua kwamba lengo la Uislamu sio kulazimisha; kwamba hauwaamuru Waislamu kunyanyua panga zao juu ya kichwa cha yeyote asiyekuwa Mwislamu na kutoa chaguo jepesi la Uislamu ama kifo.

## AMANI NA MAAFIKIANO

Kuna kundi jingine la aya linalojitokeza kwenye Qur'ani ambazo pia zinahusiana na mjadala wetu. Yote katika yote, Uislamu unatoa umuhimu mkubwa kwenye suala la amani. Katika aya moja, imeelezwa wazi kabisa:

**"Na sulhu ni bora" (4:128).** Bila shaka amani sio sawasawa na vurugu, mateso na utiifu kwa dhalimu. Katika aya nyingine tunaambiwa:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱدْخُلُوا۟ فِى ٱلسِّلْمِ كَآفَّةً .....

**""Enyi mlioamini! Ingieni katika Uislamu nyote....." (Qur'an 2:208).**

Lakini bado yenye kujieleza zaidi ni hii:

۞ وَإِن جَنَحُواْ لِلسَّلۡمِ فَٱجۡنَحۡ لَهَا وَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِۚ

**“Na kama wakielekea kwenye amani, nawe ielekee, na mtegemee Mwenyezi Mungu.....” (Qur’an 8:61).**

Hapa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anaambiwa kwamba kama wapinzani wakitetea amani, kama wakifanya juhudi yenye uaminifu kwa ajili ya amani, basi naye pia afanye amani. Kama wakipenda amani kwa uaminifu kabisa basi na yeye apende amani. Aya hizi zinaonyesha kwa uwazi kabisa kwamba msingi wa Uislamu ni ule wa amani.

Katika aya nyingine ambayo imo katika Suratun-Nisa, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) pia anaambiwa:

ۚ فَإِنِ ٱعۡتَزَلُوكُمۡ فَلَمۡ يُقَٰتِلُوكُمۡ وَأَلۡقَوۡاْ إِلَيۡكُمُ ٱلسَّلَمَ فَمَا جَعَلَ ٱللَّهُ لَكُمۡ عَلَيۡهِمۡ سَبِيلٗا

**“.....watakapojitenga nanyi, wasipigane nanyi na wakawapa amani, basi Mwenyezi Mungu hakuwafanyia njia ya kupigana nao.....” (Qur’an 8:90).**

Ewe Mtume! Kama wao wamejitoa katika vita, na wako tayari kufanya amani nanyi, basi Mwenyezi Mungu hawapi ruhusa ya kusonga mbele zaidi na kupigana nao.

Katika Sura hiyo hiyo, inaelezwa zaidi kuhusu wanafiki:

.... فَإِن تَوَلَّوْا۟ فَخُذُوهُمْ وَٱقْتُلُوهُمْ حَيْثُ وَجَدتُّمُوهُمْ ۖ وَلَا تَتَّخِذُوا۟ مِنْهُمْ وَلِيًّا
وَلَا نَصِيرًا ﴿٨٩﴾ إِلَّا ٱلَّذِينَ يَصِلُونَ إِلَىٰ قَوْمٍۭ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُم مِّيثَـٰقٌ أَوْ جَآءُوكُمْ
حَصِرَتْ صُدُورُهُمْ أَن يُقَـٰتِلُوكُمْ أَوْ يُقَـٰتِلُوا۟ قَوْمَهُمْ

**“.....Wakikataa wakamateni na muwaue popote muwakutapo, wala msifanye katika wao rafiki wala msaidizi. Ila wale waliofungamana na watu ambao baina yenu na wao mna ahadi, au wakawajia hali ya vifua vyao vina dhiki kupigana nanyi au kupigana na watu wao.....” (Qur’an 4:89-90).**

Kama wale wanafiki wanaopigana nasi wakikimbia, wanapaswa kukamatwa na kuuwawa popote watakapokuwa, sio watu wakuchukuliwa kwenye urafiki, nasi hatupaswi kukubali msaada kutoka kwao, isipokuwa kutoka kwa wale ambao wana mkataba na watu ambao sisi tuna mkataba nao, na ambao wako tayari kuja kufanya mkataba na sisi. Hawa hatupaswi kuwauwa, na wale ambao wamechoka kupigana, sisi pia hatupaswi kuwapiga.

Hivyo tumeangalia kwenye mifuatano minne ya aya. Mfuatano mmoja unaziangalia zile aya ambazo zinatuambia sisi tupigane bila masharti, kwa hiyo kama tulikuwa nayo masikio na tukawa tumesikia aya hizi tu na sio pamoja na hizo nyinginezo, ingewezekana kwetu sisi kufikiria kwamba Uislamu ni dini ya vita. Mfuatano wa pili umebeba zile aya ambazo zinatoa amri ya kupigana bali kwa masharti fulani; masharti kama vile upande wa upinzani ukiwa katika hali ya kivita na sisi, au umati wa Waislamu au wasiokuwa Waislamu wakiwa wamewekwa chini ya visigino vya kundi kutoka miongoni mwao wenyewe ambalo limekandamiza uhuru na haki zao. Mfuatano wa tatu wa aya unatuwekea wazi kabisa kwamba

wito wa Uislamu hautangazwi kwa nguvu yoyote ya silaha. Na katika mfuatano wa nne, Uislamu kwa uwazi kabisa unatangaza mapenzi yake ya amani.

# MLANGO WA TATU

## ULINZI – MSINGI WA JIHADI

Ni muhimu hapa kuelezea juu ya asili ya Jihadi. Kuna makubaliano kamili kabisa miongoni mwa watafiti kwamba msingi wa jihadi ni ulinzi. Uislamu kamwe hauruhusu kuhujumu mali na rasilimali za wengine kwa ajili ya rasilimali hizo tu. Uislamu unachukulia aina hii ya mapigano kama ni uonevu. Jihadi ni kwa ajili ya ulinzi tu, na kwa kweli ni upinzani dhidi ya uvamizi, na kwa hakika unaweza kuwa ni halali kisheria. Bila shaka, kuna pia uwezekano wa aina ya tatu ambao kwamba mtu anaweza akapigana sio kwa ajili ya uvamizi, wala si katika ulinzi binafsi, bali kwa ajili ya upanuzi wa thamani ya binadamu. Huu utajadiliwa baadaye. Katika maelezo ya msingi ya jihadi, hakuna tofauti ya maoni na watafiti wote wanakubaliana kwamba jihadi lazima iwe ni kwa ajili ya ulinzi. Tofauti za maoni zilizopo ni ndogo sana, na zinahusu swali la hilo jambo ambalo linapaswa kulindwa.

### AINA ZA ULINZI

Maoni ya baadhi ya wanachuoni juu ya jihadi yamekomea kwenye kujilinda mwenyewe, yaani, vita ni halali kwa ajili ya mtu mmoja, kabila au taifa pale inapokuwa ni kwa ajili ya ulinzi wake na uhai wake. Kwa mujibu wa maoni haya, endapo maisha ya watu yamo hatarini kutokana na eneo jingine hasimu, hapo kupigana kwa ajili ya ulinzi wa maisha na uhai wao ni halali kwa watu kama hao. Kwa namna hiyo hiyo, kama mali yao inakabiliwa na uvamizi, basi kuto-

kana na mtazamo wa haki za binadamu, wao wana haki ya kulinda mali zao ambazo ni haki yao. Kadhalika, kama watu wanakabiliwa na uchokozi wa taifa jingine linalotaka kutwaa umiliki wa utajiri wao na pengine kuubeba na kuuhamisha, basi hapo watu hao wanayo haki ya kutetea na kulinda utajiri wao, hata kwa nguvu.

المقتول دون أهله و عياله شهيد

**"Yeyote anayeuwawa wakati wa kutetea mali au heshima yake huyo amekufa Shahidi."**

Uislamu unatuambia kwamba yeyote anayeuwawa wakati wa kutetea mali au heshima yake huyo amekufa Shahidi. Kwa hiyo, katika Uislamu, mtu kulinda heshima yake ni kama kutetea uhai na mali yake. Kwa kweli hilo ni bora. Ni ulinzi wa heshima yake mtu. Kwa taifa, kulinda uhuru wake, ni halali isiyopingika. Hivyo, wakati kundi linapotaka kuchukua uhuru wa taifa na kuliweka taifa hilo chini ya utawala wake, kama watu wa taifa hilo linalochokozwa wakiamua kujilinda wenyewe na wakabeba bunduki, kitendo hiki ni halali kabisa, cha kusifiwa na kinachostahiki kupendwa. Hivyo ulinzi wa uhai, ulinzi wa utajiri, mali na ardhi, ulinzi wa uhuru na ulinzi wa heshima ni aina za ulinzi halali. Hakuna anayetilia shaka ukweli kwamba katika hali kama hizi ulinzi na kujitetea kunaruhusiwa. Kama tulivyokwisha kusema, mawazo ambayo baadhi ya Wakristo wanayatoa kuhusu dini kupaswa kuhubiri amani na sio vita, na kwamba vita ni vibaya kabisa, na kwamba amani ni nzuri sana, hayana msingi wa kimantiki au wa kiakili wa kuweza kuungwa mkono. Sio tu kwamba kupigana kwa ajili ya ulinzi sio makosa, bali kuna haki kabisa katika suala hili la kupigana na ni moja ya mahitaji muhimu ya maisha ya binadamu. Hili ndio linalomaanishwa ndani ya Qur'ani pale tunapoambiwa:

وَلَوْلَا دَفْعُ ٱللَّهِ ٱلنَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَّفَسَدَتِ ٱلْأَرْضُ

**".....Na kama Mwenyezi Mungu asingeliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, ingeliharibika ardhi....." (Qur'an 2:251)**

..... وَلَوْلَا دَفْعُ ٱللَّهِ ٱلنَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَّهُدِّمَتْ صَوَٰمِعُ
وَبِيَعٌ وَصَلَوَٰتٌ وَمَسَٰجِدُ يُذْكَرُ فِيهَا ٱسْمُ ٱللَّهِ كَثِيرًا

**".....Na lau Mwenyezi Mungu asingeliwakinga watu kwa watu, basi yangelivunjwa mahekalu na makanisa na (sehemu) za kuswalia na misikiti ambayo ndani yake hutajwa jina la Mwenyezi Mungu kwa wingi....." (Qur'an 22:40)**

## HAKI ZA BINADAMU

Kunakuwepo na swali, hata hivyo, la iwapo vitu tunavyoruhusiwa kuvilinda ni hivi tu, yaani, haki za mtu binafsi, za kundi na taifa (umma), au iwapo ni halali kwa sisi kulinda vitu vingine vile vile. Je, kuna vitu ambavyo ulinzi wake ni muhimu na wajibu, ambavyo vinafungamana tu kwenye haki za mtu binafsi, kabila au taifa, bali vinavyofungamana na binadamu wote kwa jumla? Endapo mahali fulani haki za kibinadamu zinatwaliwa visivyo haki, je, ni halali kisheria kupigana? Je vita vinavyopiganwa kwa ajili ya ubinadamu ni halali?

Pengine mtu atauliza 'Kupigana kwa ajili ya ubinadamu maana yake ni nini? Mimi sina haja ya kupigana kwa ajili ya haki yoyote

ile isipokuwa kwa ajili ya haki zangu mwenyewe binafsi, au imezidi sana, kwa ajili ya haki za taifa langu. Ninahusika nini na haki za ubinadamu? Namna hii ya fikira kwa hali yoyote ile sio sahihi.

Kunakuwepo na mambo fulani ambayo ni bora zaidi kuliko haki za mtu binafsi au taifa. Vitu au mambo fulani ambayo ni matukufu, matakatifu zaidi, ambayo ulinzi wake, kwa mujibu wa ufahamu wa kibinadamu, ni wa umuhimu wa hali ya juu kabisa kuliko ulinzi wa haki binafsi. Na haya ni yale maadili ya kuheshimika sana ya ubinadamu. Kwa maneno mengine, utukufu wa kupigana kwa ajili ya ulinzi haumo katika kujilinda mwenyewe, bali katika kutetea 'haki.' Wakati sababu na kigezo ni 'haki' inakuwa na tofauti gani iwapo ni haki binafsi au haki ya jumla ya ubinadamu? Kwa kweli utetezi wa haki za ubinadamu ni mtukufu zaidi, na ingawa hakuna anayesema hivyo, unakubalika kirahisi katika vitendo.

Kwa mfano, uhuru ni moja ya maadili matukufu ya ubinadamu. Uhuru haukomei kwa mtu mmoja binafsi au taifa. Sasa, kama sio uhuru wetu na sio uhuru wa nchi yetu, bali ni uhuru katika pembe nyingine ya dunia ndio unaoingiliwa na kuhalifiwa, je, utetezi wa haki hiyo ya kibinadamu, kwa ajili tu ya kulinda haki za binadamu ni halali kwetu sisi? Kama ni halali, basi ulinzi hauishii kwenye mipaka ya yule mtu hasa ambaye uhuru wake uko kwenye hatari, bali ni halali, na hata wajibu wa lazima kwa watu wengine na mataifa mengine kukimbilia kwenda kusaidia kupatikana uhuru, na kupigana dhidi ya mvamizi huyo wa uhuru. Sidhani kwamba kuna mtu yeyote mwenye shaka kwamba aina tukufu kabisa ya jihadi na aina tukufu kabisa ya vita ni ile ambayo inapiganwa katika kutetea ubinadamu na haki za binadamu.

Wakati watu wa Algeria walipokuwa kwenye vita na wakoloni wa Kifaransa, kikundi cha watu wa Ulaya kiliwasaidia katika vita

hivyo, ama kupitia ushiriki kwenye medani ya vita ama kwenye nyanja nyinginezo. Unadhani kwamba kule kupigana kwa Wa-Algeria tu kulikuwa ndio halali kwa sababu haki zao zilivamiwa? Ni vipi kuhusu wale watu waliotoka kwenye sehemu za mbali za Ulaya kuja kushiriki kwenye vita hivyo kusaidia taifa la Algeria? Je tuwaambie kwamba: 'Acheni kuingilia kwenu. Inakuhusuni nini ninyi? Hakuna mtu aliyeingilia haki zenu, sasa kwa nini mnapigana hapa?' Au ni kwamba jihadi ya watu kama hao ni takatifu zaidi kuliko jihadi ya watu wa Algeria wenyewe, kwa sababu Wa-Algeria walikuwa wanatetea jambo la haki zao wenyewe, wakati ambapo sababu ya hao wengine ilikuwa ya kimaadili zaidi na tukufu zaidi kuliko ile ya Wa-Algeria. Ni dhahiri kwamba lenye thamani sana ni hili wazo la pili.

Wapenda uhuru wamejipatia heshima ya jumla kutokana na kule kujitoa wenyewe kama watetezi wa haki za binadamu, sio watetezi wa haki zao binafsi au haki za taifa lao au hata za bara lao wenyewe. Kama walikuwa kamwe waende zaidi ya matumizi ya ulimi, kalamu, barua na hotuba na wakaenda hasa kwenye medani ya vita na wakapigana huko, kwa ajili ya Wapalestina kwa mfano, au Viet-Cong, hapo dunia inapaswa kuwachukulia hao kama watukufu zaidi.

Dunia inaitazama vita, wakati wowote inapokuwa ni kwa ajili ya ulinzi kuwa ni takatifu. Kama ni ulinzi binafsi inakuwa ni takatifu. Kama ni kwa ajili ya ulinzi wa nchi yake mtu, inakuwa ni takatifu zaidi kwa kuwa sababu yake imekua kutoka ile ya binafsi hadi ya taifa, na mtu huyo hajitetei yeye binafsi bali anawatetea na watu wengine pia ambao wanaunda jamii yake. Na kama utetezi ukihama kutoka kwenye taifa kwenda kwenye sababu ya ubinadamu, hapo tena inakuwa takatifu zaidi.

# MGOGORO MDOGO

Hapa tena ni asili ya mgogoro kuhusu jihadi; sio mgogoro mkubwa bali ni mgogoro mdogo. Mgogoro sio kuhusu iwapo jihadi ni halali tu katika kujilinda, mgogoro ni katika fasili au ufafanuzi wa neno ulinzi. Mgogoro huu mdogo ni kuhusu iwapo maana ya ulinzi mipaka yake ni kwenye ulinzi binafsi, zaidi sana kwenye ulinzi wa taifa lake mtu, au iwapo ulinzi wa ubinadamu pia unaingia katika kundi la mfano huu?

Baadhi ya watu wanasema, na wako sahihi, kwamba ulinzi wa ubinadamu pia ni ulinzi halali. Hivyo, njia ya wale wanaosimama ili 'kuamrisha mema na kukataza mabaya' ni takatifu. Inawezekana kwamba mtu, yeye mwenyewe hakuvamiwa au kuingiliwa, na anaweza pia kuwa anaheshimika sana na mahitaji yote ya maisha yanaweza yakawa kwake yanapatikana na hilo linaweza pia kuwa hivyo kwenye haki za mali ya nchi yake. Lakini kwa mtazamo wa maadili ya binadamu, haki ya msingi ya binadamu inaingiliwa visivyo. Kwa maana kwamba, ndani ya jamii yake, ingawa sio haki ya mali ya jamii hiyo wala haki yake binafsi ambayo imeingiliwa, bado kuna kazi inayongoja kutekelezwa katika maslahi ya ubinadamu. Yaani, wakati wema na uovu vimo katika jamii, hii ya kuamrisha mema ni lazima itekelezwe na kuwa ndio utaratibu, wakati hili la pili, uovu, lazima liondolewe.

Sasa, kwa mazingira haya, kama mtu anaona kwamba lile jema, lenye kutambulika, lenye kukubalika limeshushwa kwenye nafasi ya lililo baya, linalokataliwa, na kwamba lile linalokataliwa limechukua nafasi ya lile linalotambuliwa, na akanyanyuka kwa ajili ya kuamrisha lile linalotambulika na kukataza lile linalochukiza, basi hapo atakuwa anatetea nini? Haki zake binafsi? Hapana. Je, ni haki za msingi za jamii yake? Hapa tena ni hapana. Utetezi wake

hauhusiani na haki za mali. Anachokitetea ni haki za kiroho ambazo sio za mtu mmoja au taifa; ni haki ya kiroho inayohusika na watu wote wa dunia. Je, tunapaswa kushutumu au kulaumu jihadi ya mtu huyo au tuichukulie kuwa ni takatifu? Ni dhahiri kabisa kwamba tunapaswa kuichukulia kuwa ni takatifu, kwani iko katika utetezi wa haki ya ubinadamu.

Juu ya suala la uhuru, unaona leo hii kwamba watu wale wale wanaopambana na uhuru, ili kujipatia wao wenyewe hali ya kuheshimika, ndio wanaodai kuwa watetezi wa uhuru, kwani wanajua kwamba utetezi wa uhuru hata bila kusema unaeleweka kama ni mtakatifu. Kama wangekuwa kweli wanapigana kwa ajili ya kutetea uhuru, hili lingekuwa sahihi, lakini wao wanaupa uvamizi wao wenyewe jina la utetezi wa uhuru. Hata hivyo, kitendo chao ni ukubalikaji wa ukweli kwamba haki za ubinadamu zinastahili kutetewa na kulindwa, na kwamba vita kwa ajili ya kutetea haki hizo ni halali na vyenye manufaa.

## TAWHIID (IMANI YA MUNGU MMOJA): NI HAKI BINAFSI AU NI YA WOTE?

Sasa jambo moja muhimu sana lazima liangaliwe, ambalo ni kuhusu 'Tawhiid.' '*La illaha illallah.*' Yaani 'Hakuna mungu ila Allah – Mwenyezi Mungu.' Je, Tawhiid inafungamana na haki za wanadamu, au kwenye haki za mtu binafsi? Hapa, inawezekana kusema kwamba Tawhiid haifungamani na haki za wanadamu wote bali inafungamana na mambo ya mtu binafsi tu, au kwa zaidi sana, kwenye mambo ya ndani ya taifa. Kwamba yeye mwenyewe anaweza kuwa '*muwahid*' 'mwenye imani ya Mungu Mmoja', Ana uamuzi wa kuwa '*muwahid*' akitaka kuwa hivyo, au '*mushrik*' mshirikina,

kama akitaka kuwa hivyo, na sasa kwa kuwa amekuwa *muwahid*, hakuna mwenye haki ya kumsumbua yeye; hiyo ni haki yake binafsi, na kama mtu mwingine anakuwa *mushrik*, basi hiyo ni haki ya mtu huyo.

Taifa moja lolote katika sheria zake linaweza kuchagua moja ya nafasi tatu; kuchagua Tawhiid na kuitwaa kama dini rasmi na kukataa rasmi dini nyingine yoyote; kukubali ushirikina kama dini rasmi, au kuruhusu uhuru wa ibada. Mtu anaweza kuchagua dini yoyote au itikadi anayoitaka. Kama Tawhiid imejumuishwa katika sheria za nchi, basi ni moja ya haki za taifa hilo na kama haikujumuishwa, hapana, sio haki yake. Hii ni njia mojawapo ya kuangalia mambo. Kuna wazo jingine hata hivyo, ambalo linaichukulia Tawhiid kama uhuru, na inayofungamana na haki za binadamu. Wakati tukijadili uhuru, tulisema kwamba maana ya haki ya uhuru hairejelei tu kwenye uhuru wa mtu binafsi na kwamba haupaswi kuhatarishwa kutoka upande wowote, kwani inawezekana kuhatarishwa na mtu huyo huyo mwenyewe. Kwa hiyo, taifa linapopigania Tawhiid kupambana na ushirikina, kupigana kwake huko kunasababishwa na ulinzi, sio kwa kutiisha, udhalimu na uvamizi. Hili basi hasa ndio asili ya tofauti ndogo inayozungumziwa.

Hata miongoni mwa wanachuoni wa Kiislam kuna maoni namna mbili. Kwa mujibu wa baadhi yao, Tawhiid inafungamana na haki za jumla za binadamu, hivyo kwamba kupigana kwa ajili ya Tawhiid ni halali kisheria, kwani ni ulinzi wa haki ya binadamu na ni kama kupigana kwa ajili ya uhuru wa taifa jingine. Kundi jingine hata hivyo, linapinga na kusema kwamba Tawhiid inafungamana na haki binafsi na pengine na haki za taifa, lakini haihusiani chochote na haki za binadamu, na kwa hiyo, hakuna mwenye haki ya kumbughudhi mtu yeyote kwa ajili ya Tawhiid. Ni yapi kati ya maoni mawili haya liko sahihi?

Ninadhamiria kuelezea maoni yangu mwenyewe binafsi juu ya mada hii. Lakini kabla ya kufanya hivyo, ningependa kuzungumzia kuhusu jambo lenyewe, na pengine kwa kufikia hitimisho, mambo yote mawili yatakuja kuonekana kama ni jambo moja. Suala ni kwamba, baadhi ya mambo yanaweza yakakubalika chini ya vitisho, yaani, kukubalika kwa kulazimishwa, ambapo baadhi ya mengine, kulingana na asili yao, ni lazima yachaguliwe kwa uhuru na hiari kabisa.

Fikiria moja kwa mfano, kuathiriwa kwa hatari kabisa na ikabidi kukubali kupigwa sindano. Katika hali kama hiyo, yule anayehusika anaweza akalazimishwa kupigwa hiyo sindano, na kama mtu huyo atakataa, basi mikono na miguu yake inaweza kufungwa kwa nguvu; na kama ataendelea kukataa, sindano hiyo anaweza kupigwa wakati akiwa hana fahamu. Hili ni jambo ambalo linaweza kukubalika chini ya vitisho. Ukubalikaji wa mambo mengine hata hivyo, hauwezi kulazimishwa kwa kupitia ushurutishwaji, kwani mbali na njia ya uchaguzi huru, hakuna njia nyingine ambayo kwayo yanaweza kukubalika. Miongoni mwa mambo kama hayo tunaukuta utakasaji wa nafsi (self-purification) kwa mfano, na usafishaji wa tabia ya mtu. Kama tukitaka kuwasafisha watu ili waweze kuja kutambua na kukubali maadili kama ni wema na maovu kama ni mabaya na kujiepusha na tabia za kibanadamu zenye kasoro ili kwamba hatimaye waje kukataa upotovu na kuikumbatia haki na ukweli, hatuwezi kufanya hivyo kwa mabavu.

Inaweza ikawa rahisi kumzuia mtu asiibe kupitia adhabu, lakini haina nguvu katika kutengeneza uaminifu kwa mtu. Kwani mambo kama hayo yangekuwa yanawezekana, basi kwa mfano, kama nafsi ya mtu ingekuwa yenye kuhitaji utakaso na tabia yake binafsi ina ukosefu mkubwa wa unyofu mzuri na maadili, viboko mia moja atakavyochapwa vingeweza kufanya mtu huyo kuwa mwenye

tabia na maadili mema. Badala ya elimu nzuri na bora, walimu kwa urahisi tu wangetumia kiboko na kusema: ‘Ili mtu huyu katika uhai wake wote, wakati wote aseme kweli na kuuona uongo kama jambo la kuepukwa, anapaswa kupigwa viboko mia moja, na baada ya hapo kamwe hatasema uongo tena.’ Kadhalika jambo kama hilo linatumika kwenye upendo. Je, mtu anaweza kulazimishwa kumpenda mtu mwingine kwa viboko? Upendo na mahaba haviwezi kulazimishwa mtu. Hakuna nguvu katika dunia, ambazo hata kama zingekusanywa pamoja zinazoweza kumlazimisha mtu kuwa na upendo, wala kuweza kuondoa upendo alionao juu ya mwingine.

Baada ya kuliweka wazi jambo hili, ningependa kusema kwamba imani, bila ya kujali iwapo kama ni haki ya msingi ya binadamu au hapana, ni jambo ambalo kwa asili yake hasa haliwezi kulazimishwa mtu. Kama tukitaka kujenga imani, ni lazima tuelewe kwamba haiwezekani kuijenga kwa mabavu. Imani ina maana ya itikadi na mwelekeo. Imani ama dini ina maana ya kuvutika kwayo, na kukubali seti ya itikadi. Kuvutika kwenye itikadi kuna shuruti mbili. Moja ni kwamba jambo lenyewe lazima likubaliane na akili, huu ndio mwelekeo wa kisayansi wa imani. Mwingine ni mwelekeo wa kihisia, yaani moyo wa binadamu unapaswa kuvutiwa kwenye imani. Si hisia au akili inayoweza kuingia ndani ya eneo au uwanja kwa nguvu. Sio lile sharti la kwanza, kwa sababu kufikiri kunategemea mantiki, kama ikipendelewa kwamba mtoto afundishwe ufumbuzi wa swali la kihesabu, ni lazima afundishwe katika njia ya kimantiki ili kwamba agundue usadikisho ndani yake. Hawezi kufundishwa kwa kiboko. Akili yake haitaweza kulikubali jambo kwa njia ya mabavu au kichapo. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo kwa hili sharti la pili, hali ya kihisia, ambayo inaibua mwelekeo, mvuto na silika.

Kwa mujibu wa hili, kuna tofauti kubwa sana kati ya Tawhiid kama haki ya binadamu na zile haki nyingine za kibinadamu kama

vile uhuru. Uhuru ni jambo ambalo linaweza kuwekwa juu ya watu kwa nguvu, kwa sababu uvamizi na ukandamizaji vinaweza kuzuiwa kwa kutumia nguvu. Lakini kuishi huru na moyo wa kupenda uhuru ni mambo ambayo hayawezi kuwekwa juu ya watu kwa nguvu. Haiwezekani kumlazimisha mtu kukubali itikadi au kujenga imani kwa mabavu katika moyo wake juu ya jambo fulani. Hii ndio maana ya ”Hakuna kulazimisha katika dini.” Pale Qur’ani inaposema kwamba hakuna kulazimisha katika dini, haina maana kwamba, ingawa inawezekana kwa dini kuamrishwa kwa nguvu, tusiiamrishe na tuwaache watu kutwaa dini yoyote wanayotaka. Hapana. Kile inachokisema Qur’ani ni kwamba dini haiwezi kuamrishwa. Kama ikiamrishwa kwa lazima hiyo sio dini.

Kwa wale Mabedui wa Kiarabu, ambao waliikubali dini bila kuielewa asili ya msingi wake, na bila Uislam wenyewe kuwa umeziathiri nyoyo zao, ambao walidai kwamba ’wameamini,’ Qur’ani ilitoa majibu haya:

۞ قَالَتِ ٱلْأَعْرَابُ ءَامَنَّا ۖ قُل لَّمْ تُؤْمِنُوا۟ وَلَـٰكِن قُولُوٓا۟ أَسْلَمْنَا وَلَمَّا يَدْخُلِ ٱلْإِيمَـٰنُ فِى قُلُوبِكُمْ

**“Mabedui walisema: Tumeamini. Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu. Kwani imani haijaingia katika nyoyo zenu.....” (Qur’an 49:14)**

Katika istilahi ya Qur’ani neno ’Waarabu’ linarejelea kwa mabedui wahamaji wa jangwani. Mabedui hao walikuja kwa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) wakidai kwamba wameamini. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliagizwa awaambie kwamba walikuwa hawana imani ya kweli, na kwamba wao wamesilimu tu, yaani

wamefanya tamko la maneno ya mdomoni, linalowapa haki ya juu juu ya kuchukuliwa kama ni Waislamu, walitamka ”La illaha illallah, Muhammadan rasulullah’ kauli inayowapa haki zilezile alizonazo Mwislamu. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa awaambie hata hivyo kwamba imani bado ilikuwa haijaingia katika nyoyo zao.

وَلَمَّا يَدۡخُلِ ٱلۡإِيمَـٰنُ فِي قُلُوبِكُمۡ

**“..... Kwani imani haijaingia katika nyoyo zenu.....” (Qur’an 49:14)**.

Hili linatuambia kwamba imani inahusiana na moyo.

Kipengele kingine kinachounga mkono madai yetu ni kwamba Uislamu hauruhusu taqliid (uigizaji) katika kanuni za misingi ya dini na unahesabu uchunguzi huru kuhusiana na hili kuwa ni muhimu sana. Kanuni za misingi ya dini bila shaka zinahusiana na itikadi na imani. Hivyo inajitokeza wazi kwamba, katika Uislamu, imani ni matokeo ya mawazo huru. Imani na itikadi ambazo Uislamu unazilingania haziwezi kupatikana kwa kupitia ‘taqliid’, au nguvu na ushurutishwaji.

Sasa tunayatambua maoni namna mbili ya watafiti wa Kiislamu kuwa yanakaribiana sana. Kundi moja linatoa hoja kwamba Tawhiid inafungamana na haki za kilimwengu za ubinadamu na kwa sababu ni uhalali usiopingika wa kutetea haki za binadamu, hivyo ni halali kutetea Tawhiid na kupigana dhidi ya wengine kwa ajili yake. Hilo kundi jingine linadai kwamba hakuna kabisa njia halali ya kupigana kwa ajili ya Tawhiid, na kama taifa ni la kishirikina, haturuhusiwi kulipiga kwa sababu hiyo tu. Sasa ukaribu wa maoni yote umeegemea kwenye ukweli kwamba, hata kama tukichukulia kwamba Tawhiidi ni haki ya kibinadamu, bado hatuwezi kupigana na

taifa jingine ili kulazimisha imani ya Tawhiid juu yao, kwani kama tulivyoona, kwa hali yake hasa ya msingi wake, Tawhiid sio jambo ambalo linaweza kulazimishwa. Kuna mtazamo mwingine pia, yaani kama tukichukulia Tawhiid kama haki ya binadamu na kama tukiona kwamba ni kwa manufaa bora ya binadamu, basi tunaruhusiwa kupigana na taifa la washirikina. Lakini vita vyetu visije vikalenga katika kulazimisha Tawhiid na imani juu yao kwa vile tunajua kwamba Tawhiidi na imani haviwezi kulazimishwa. Tunaweza hata hivyo kuwapiga washirikina ili kung'oa maovu katika jamii hiyo, lakini haturuhusiwi kulazimisha itikadi ya Tawhiidi juu yao.

Kwa mujibu wa wale wanaoiona Tawhiid kuwa inafungamana na haki za mtu binafsi ama zaidi sana kwenye haki za taifa, hairuhusiwi kuanzisha vita kwa ajili ya kuung'oa ushirikina. Mwelekeo wa fikra wenye nguvu sana huko Magharibi, ambao pia umepenya kwenye safu za Waislamu ni huu hasa. Masuala kama Tawhiid yanaonekana kwa watu wa Ulaya kama mambo binafsi na hayana umuhimu kabisa katika maisha; takriban wanachukulia kama ni desturi ambayo kila taifa lina haki ya kuchagua. Kwa hiyo, hata kwa ajili ya kung'oa maovu, hakuna mwenye haki ya kupambana na ushirikina, kwa sababu ushirikina sio uovu, na Tawhiid ni suala la binafsi moja kwa moja.

Kama, kwa upande mwingine, tukiichukulia Tawhiidi kama jambo la wote, linalofungamana na haki za binadamu na ustawi na mafanikio ya jumla ya binadamu, hapo inaruhusiwa kuanzisha vita juu ya washirikina kwa ajili ya utetezi wa Tawhiid na ili kung'oa dhulma. Hata hivyo, vita kwa ajili ya kulazimisha Tawhiid hairuhusiwi.

Kuna jambo jingine ambalo linapaswa kuelezwa, yaani kupigana kwa ajili ya uhuru wa huo 'wito.' Ni lazima tuwe na uhuru wa kutoa ujumbe wa imani na itikadi fulani kwa taifa lolote lile. Kama

tunachukulia uhuru kuwa ni haki ya binadamu ya kilimwengu, au Tawhiid kuwa kama hivyo, au yote mawili kuwa ni haki ya binadamu kwa ulimwengu mzima, kuanzisha vita kwa ajili ya uhuru wa wito huo ni dhahiri kwamba ni halali. Sasa, kama pingamizi linaibuka dhidi ya wito wetu, kama mamlaka fulani, tuseme kwa mfano, ikijitokeza yenyewe kama kikwazo, ikitunyima sisi ruhusa, ikisema kwamba wito huo utaharibu akili ya umma wake, na tunajua kwamba serikali zote zinaona kama ni kuharibu fikira zote ambazo zinaweza kuwahimiza watu kufanya maasi dhidi yao, na inajiweka yenyewe kama kikwazo kwenye wito wa haki, je, inaruhusiwa kupigana nayo hadi ianguke na kikwazo dhidi ya wito huo kivunjike?

Ndio, hili pia linaruhusiwa. Hili litakuwa kwa ajili ya njia ya ulinzi. Hili litakuwa ni moja ya zile jihadi, ambazo asili yake hasa ni ulinzi.

## KIGEZO CHA KUTATHMINI HAKI BINAFSI NA HAKI YA WOTE

Mpaka hapa tumeona kwamba msingi wa Jihadi ni ulinzi. Sasa tunapaswa kuona iwapo kama Tawhiid inafungamana na haki za wote za ubinadamu, au na haki za mtu binafsi, au zaidi sana, kwenye haki za taifa. Tunachopaswa kufanya ni kuangalia kigezo kwa ajili ya haki binafsi, haki za wote za ubinadamu. Katika baadhi ya mielekeo wanadamu wote ni sawa, ambapo katika mingine wako tofauti. Binadamu wanatofautiana kwa namna nyingi kiasi kwamba watu wawili hawawezi kupatikana, ambao katika kila maelezo wako sawasawa kabisa. Watu wawili wenye sifa za kimaumbile za sawasawa hawapo. Ni kweli pia kwamba hakuna watu wawili wenye sifa sawa za kiroho. (Sifa za wote zinahusiana na) mahitaji na haja za kawaida

za binadamu wote. Uhuru maana yake ni kutokuwepo kwa vikwazo kwenye upambaji wa uwezo wa asili wa mtu binafsi, na unahusiana na binadamu wote. Uhuru kwa ajili yangu una thamani ile ile hasa kama uliyonao kwa ajili yako. Una thamani ile ile hasa kwako wewe kama ilivyo kwa wengine. Kati yako wewe na mimi hata hivyo, zipo tofauti nyingi sana, na hizi zinafungamana na 'shaksia' kwa sababu ni tofauti za kibinafsi. Kama rangi na umbile vinavyotofautiana katika binadamu, shaksia zao vile vile hutofautiana. Ninaweza nikapenda nguo za rangi fulani ambapo wewe ukapenda za rangi tofauti. Naweza nikapenda kuishi kwenye mji mmoja ambapo wewe ukapenda kuishi kwenye mwingine. Ninaweza kupanga na kupamba nyumba yangu kwa njia moja, ambapo wewe ukachagua njia tofauti. Naweza nikachagua somo moja la kujifunza na wewe ukachagua jingine tofauti na hilo.

Hivi vyote ni vipaji binafsi ambavyo kwamba hakuna mtu anayeweza kubughudhiwa kwavyo. Hivyo hakuna mwenye haki ya kumlazimisha mtu kuoana na mtu fulani, kwani ndoa ni jambo binafsi na katika kuchagua mwenza wa ndoa kila mtu ana vionjo vyake binafsi. Uislamu unasema kwamba mtu yeyote asilazimishwe katika kuchagua mwenza wake, wa kiume au wa kike, kwa sababu fursa hii iko ndani ya haki binafsi ya mtu mwenyewe. Wazungu ambao wanasema kwamba mtu yeyote asibughudhiwe kwa ajili ya Tawhiid au imani, wanasema hivyo kwa sababu wanadhani kwamba dhana hizi mbili zimo miongoni mwa mambo binafsi ya mtu. Kwao wao, dini ni kitu kinacholeta burudani kwa wanadamu wote.

Katika mtazamo wa maoni yao, ni kama sanaa: mtu mmoja anampenda Hafidh na mwingine anampenda Sa'adi, mwingine Firdaus. Mtu yeyote asimbughudhi yule anayempenda Sa'adi, akisema: 'Kwa nini unampenda Sa'adi? Mimi ninampenda Hafidh. Na wewe pia unapaswa kumpenda Hafidh.' Kwao wao dini inakomeshea

kwenye mpaka huu. Mtu mmoja anachagua Uislamu, ambapo mwingine anachagua Ukristo, mwingine anachagua Uzoroastria, ambapo bado mwingine hashughulishwi japo kidogo na dini hizo zote. Hakuna yeyote anayelazimika kusumbuliwa kwa hilo. Dini katika mtazamo wa Wazungu hawa haihusiani na kiini cha maisha, na njia ya maisha ya binadamu. Hii ndio dhana yao ya msingi, na kati ya mwelekeo wao wa fikra na wa kwetu kunakuwepo na tofauti nyingi sana. Kwetu sisi, dini ina maana ya 'Njia iliyonyooka' ya wanadamu na kupuuza dini maana yake ni kupuuza njia iliyonyooka, kupuuza ile njia halisi ya maendeleo ya binadamu.

Tunasema kwamba Tawhiid ni nguzo ya ustawi, ufanisi na furaha ya binadamu. Sio tu jambo binafsi la mtu au jambo pekee la kundi hili au lile. Hivyo, ukweli uko pamoja na wale wanaoamini kwamba Tawhiid inafungamana na haki za binadamu. Endapo, kwa wakati huo huo, tunasema kwamba vita kwa ajili ya kulazimisha Tawhiid haviruhusiwi, sio kwa sababu Tawhiid inafungamana na mambo hayo ambayo sio lazima yatetewe na sio haki za ulimwengu za binadamu wote, bali ni kwa sababu asili yenyewe hasa ya Tawhiid hairuhusu yenyewe kulazimishwa, kama Qur'ani inavyothibitisha hilo: 'Hakuna kulazimisha katika dini.'

## UHURU WA MAWAZO AU UHURU WA IMANI?

Nukta nyingine ambayo ni lazima isisitizwe hapa ni kwamba kuna tofauti kati ya 'uhuru wa mawazo' na 'uhuru wa imani' Wanadamu wamejaaliwa na uwezo wa fikira ambao unawawezesha wao kufanya maamuzi kwa msingi wa kufikiri, mantiki na hoja. Lakini imani inahitaji fungamano lenye nguvu kwenye lengo la imani yenyewe. Nyingi ni imani ambazo haziegemei kwenye fikira, bali ni uigizaji

mtupu, ni matokeo ya malezi na tabia, na ambayo pia hukera uhuru wa binadamu. Tunasema kwamba binadamu lazima awe na uhuru wa mawazo. Bado kuna baadhi ya imani ambazo hazina mizizi japo kidogo kwenye fikira; zina mizizi yao katika ubwete mtupu na udororaji wa moyo, uliopokelewa kutoka kizazi hadi kizazi; zenyewe ni namna ya kifungo au utumwa. Hivyo vita vyovyote vitakavyopiganwa kwa ajili ya kuondoa imani kama hizo ni vita vilivyopiganwa kwa ajili ya uhuru wa binadamu, sio vita dhidi yake. Kama mtu ataomba kwa ajili ya mahitaji yake kwa sanamu alilolitengeneza mwenyewe, basi katika maneno ya Qur'ani, mtu huyo ni duni kuliko mnyama. Hii ina maana kwamba, kile kitendo cha mtu huyu hakikutegezwa hata kidogo kwenye fikira. Kufikiri japo kidogo kusingemruhusu kujiingiza kwenye kitendo kama hicho. Matendo yake ni uakisi mtupu wa udororaji na mbweteko ambavyo vimejitokeza kwenye moyo wake na katika nafsi yake, na ambavyo vimejikita kwenye uigizaji wa upofu. Mtu huyu ni lazima akombolewe kwa nguvu kutoka kwenye minyororo ya ndani ambayo inamfunga, ili kumuwezesha kufikiri. Hivyo, wale wanaouelezea uhuru wa kuigiza na uhuru wa juu juu ambao kwa kweli unazifunga nafsi kama ndio uhuru wa imani, kwa kweli hao wamekosea kabisa. Tunachokipigania, kwa mujibu wa hii aya: 'Hakuna kulazimisha katika dini' ni ule uhuru wa mawazo, uhuru wa kufikiri.

# MLANGO WA NNE:

## SUALA LA UTANGUAJI (UBATILISHAJI)

### UTANGUAJI

Mjadala wetu ulikuwa ni juu ya Jihadi ya Kiislamu. Kuna mambo matatu ambayo napenda kuyazungumzia katika mlango huu: Moja lina msingi wa Qur'ani, na jingine mantiki ndio msingi wake na la tatu lina msingi wa Qur'ani na wa kihistoria. Jambo ambalo lina msingi wa ki-Qur'ani linahusiana na aya za Qur'ani kuhusu jihadi. Tumekwisha kusema tayari kwamba baadhi ya hizo aya za jihadi ni zenye amri kamili, ambapo nyingine ni zenye masharti. Aya zenye amri kamili zinapendekeza kupigana na washirikina au Watu wa Kitabu bila ya masharti yoyote yale. Zile aya zenye masharti zimetoa amri inayoambatana na masharti maalum. Kwa mfano, imeelezwa kwamba ni lazima tupigane nao endapo wakitupiga, au kama wapo katika hali ya kivita pamoja nasi, au kama tunayo sababu ya kuhofia kutokea kwa shambulizi kutoka kwao. Kwa mujibu wa wanachuoni wa Kiislamu, aya zenye masharti ni maelezo ya zile zenye amri kamili isiyo na sharti. Hivyo ni lazima tuitafute maana ya jihadi kutoka kwenye kile kilichoelezwa na aya zenye masharti, ambavyo ina maana kwamba hizo aya za Qur'ani haziitambui jihadi yoyote isiyo na masharti kuwa ni ya wajibu.

Tena, baadhi ya wafasiri wameleta suala ya utanguaji. Wanakubali kwamba aya nyingi za Qur'ani zinaweka masharti kwa ajili ya

kupigana dhidi ya wasio Waislamu, lakini wanasema kwamba aya nyingine zimeshushwa ambazo zinatangua maelekezo na masharti yote hayo. Hivyo, tunalijia suala la utanguaji.

Baadhi ya aya zinatangua aya nyingine. Baadhi ya wanachuoni wanaamini kwamba ile aya ya kwanza ya Tawhiid katika sura ya Qur'ani inabatilisha aya za jihadi zilizotangulia. Katika aya hii tunakutana na amri ya jumla ya jihadi, kujikomboa kutoka kwa washirikina, kuweka kipndi kwa ajili yao kuishi mjini Makka ambacho baada yapo hawaruhusiwi tena kuishi humo, na wanapaswa kuzingirwa na kuuawa. Aya hii ilishuka katika mwaka wa 9 Hijiria. Je aya hii inaweza ikazibatilisha aya zilizotangulia kabla yake? Hapana. Haiwezi ikazibatilisha aya zilizotangulia kwa sababu mbili. Kwanza tunaweza tu kuichukulia aya kuwa imetangua nyingine pale itakapokuwa inapingana nayo. Fikiria aya iliyoshushwa ikiamrisha kutokupigana na washirikina kabisa ikifuatiwa na nyingine inayotoa ruhusa ya kupigana nao. Hii itamaanisha kwamba Mwenyezi Mungu ameyafuta maagizo yaliyotangulia. Hii ndio maana ya utanguaji: maagizo ya awali yanabatilishwa na kuchukuliwa nafasi yake agizo jingine. Kwa hiyo hili agizo la pili lazima liwe kwa namna ya kwamba linapingana kabisa na lile la awali. Hata hivyo, kama kwa pamoja, muktadha wa aya ya kwanza na ile ya pili unakubaliana, hivyo hiyo inaifafanua ile nyingine, basi hakuna swala la ziada la mojawapo kuwa yenye kutangua na hiyo nyingine kuwa ni yenye kutanguliwa.

Hizo aya za Surat-Tawba sio za namna ambayo kwamba zinaweza zikasemwa kwamba zimeshushwa ili kubatilisha zile zilizoshuka kabla ambazo zilikuwa zimeambatana na masharti kwenye jihadi. Kwa nini isiwe hivyo? Kwa sababu, wakati tunapozitazama aya za Surat-Tawba kwa pamoja, tunaona kwamba zinatuambia sisi tuwapige washirikina kwa sababu wao hawafuati moja ya kanuni za

misingi ya binadamu – kuchunga ahadi yake mtu – ambayo kila mtu anafahamu kwamba ni lazima ichungwe, hata kama sheria ya moja ya taifa maalum haisisitizi wajibu huu au kuijali hata kidogo. Hivyo aya hizo zinatuambia tupigane, kwa sababu kama tukiwekeana mkataba nao, wakati wowote wanapoona fursa ya kuuvunja, wao watafanya hivyo na kujitahidi kutuangamiza na kutumaliza kabisa.

Hapa busara inatuambia nini? Kama tunajua kwa uhakika kwamba kuna taifa linalokusudia kutuangamiza sisi, kwa fursa yoyote ya kwanza litakayoipata, hivi busara inatuambia tusubiri wao wafanye hivyo kabla hatujafanya lolote kuhusu hilo? Kama tukisubiri, basi wao watatuangamiza. Katika dunia ya leo, tunaweza tukaona taifa likishambulia taifa jingine kwa sababu ya ushahidi wa dhahiri kwamba hilo taifa jingine limefanya uamuzi wa kushambulia lile jingine, na wakati taifa hilo linaposhambulia, dunia yote itasema hiyo inaruhusiwa. Hakuna atakayesema kwamba ingawa walijua na walikuwa na ushahidi wa wazi kwamba, kwa mfano, adui alikuwa na nia ya kushambulia katika siku fulani, bado walikuwa hawana haki ya kumshambulia adui leo, kwamba wangepaswa kusubiri na silaha zilizohifadhiwa tayari mpaka adui atakaposhambulia na ni wakati huo tu.

Qur'ani katika aya hizo hizo za Surat-Tawba (Baraat), aya kali zaidi za Qur'ani zinatuambia:

كَيۡفَ وَإِن يَظۡهَرُواْ عَلَيۡكُمۡ لَا يَرۡقُبُواْ فِيكُمۡ إِلاًّ وَلَا ذِمَّةً ۚ
يُرۡضُونَكُم بِأَفۡوَٰهِهِمۡ وَتَأۡبَىٰ قُلُوبُهُمۡ

**"Itakuwaje! Nao wakishinda hawaangalii kwenu ujirani wala ahadi. Wanawafurahisha kwa midomo yao tu, bali nyoyo zao zinakataa..." (Qur'an 9:8)**

Inatuambia kwamba, kama wakipata fursa, wao hawachungi ahadi wala makubaliano, na chochote wanachokisema kinaishia kwenye maneno ya midomoni tu, ambapo nyoyo zao zinapinga. Hivyo aya hizi sio zisizo na masharti hivyo kama ilivyofikiriwa. Zinachokisema hasa ni kwamba, wakati tunapohisi hatari kutoka kwa maadui, kwetu sisi kukunja mikono na kuchelewa kutakuwa ni makosa. Hivyo ni lazima tusifikiri kwamba aya hizi hazikubaliani kabisa na aya zingine. Hivyo hazipaswi kuchukuliwa kama zenye kubatilisha. Hii ndio sababu ya kwanza ya kwa nini aya hizi sio zenye kubatilisha.

## HAKUNA UJUMLA BILA KUWEPO UPEKEE

Sababu ya pili iliyotolewa na wanachuoni inahusiana na maneno haya:

ما مِن عامّ إلاّ وقَد خُصَّ

**'Hakuna ujumla bila kuwepo upekee'**

Na hili ni sahihi kabisa. Tunaambiwa tufunge (saumu), lakini sio wakati tunahukumiwa kama wasafiri au wagonjwa. Hata sheria hii hii hasa ina uhalisia wake. Kuna baadhi ya ujumla ambao kwa kweli hauna upekee na wala hauruhusu upekee wowote.

Masuala mengine yanakataa kubatilishwa, yanakataa upekee (kuacha mengine). Mwelekeo wa kauli hizi za ujumla ni kwamba

haziwezi kukubali kuingiza na mengine ya upekee. Kwa mfano, katika Qur'ani tunaambiwa:

..... وَإِن تَشۡكُرُواْ يَرۡضَهُ لَكُمۡ .....

**'.....Na mkishukuru atawaridhia....." (Qur'an 39:7)**

Na kwa hili hapawezi kuwa na upekee kamwe. Haiwezekani kwamba kutakuwa na wakati ambapo mtu atamshukuru Mwenyezi Mungu kwa dhati kabisa na kisha Yeye Mwenyezi Mungu asimridhie.

Kadhalika kuhusiana na ubatilishaji, baadhi ya aya zipo kwa namna ambayo kimsingi ubatilishaji hauwezi kufanyika juu yazo kwa sababu maana ya ubatilishaji ni kwamba ile amri iliyobatilishwa ilikuwa ni ya muda. Hii ina maana kwamba mambo fulani hayakubali kuwa ya muda. Kwa mfano, hebu tuchukulie ile aya ya Qur'ani inayotuambia:

..... وَلَا تَعۡتَدُوٓاْۚ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُحِبُّ ٱلۡمُعۡتَدِينَ

**'.....wala msichokoze, kwa hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wachokozi....."**

Hii ina ujumla kuhusiana na watu na uendelevu kuhusiana na wakati. Je, inawezekana kwetu sisi kutwaa upekee kwenye ujumla huu? Hivi tunaweza kusema kwamba Mwenyezi Mungu hawapendi madhalimu isipokuwa wachache? Utukufu wa Mungu kwa upande mmoja na uchafu wa dhulma na uonevu kwa upande mwingine haviwezi kwenda pamoja. Hatuwezi kusema kwamba Mwenyezi

Mungu hawapendi wachokozi isipokuwa fulani. Huu ni ujumla ambao haukubali upekee. Hii sio sawa na kufunga ambapo tunasema ni lazima tufunge isipokuwa tunapokuwa kwenye hali hii na ile. Kuhusiana na funga ya saumu, inawezekana kwamba katika hali fulani, mtu lazima asifunge, lakini hatuwezi kusema kwamba katika wakati mmoja lazima tuwe madhalimu na katika mwingine tusiwe hivyo. Popote pale palipo na dhulma na uonevu, ni makosa na ni uhalifu, bila ya kujali ni nani aliyeutenda. Hata kama ingekuwa ni Mitume wa Mwenyezi Mungu waliofanya hayo, bado ingekuwa ni hatia ya kulaumika, na kuchukuliwa kama ni dhambi na ukosefu wa utii. Mwenyezi Mungu hampendi yeyote asiye mtiifu. Hata kama ingekuwa Mitume (Mwenyezi Mungu anisamehe kwa mawazo haya) wangetenda dhambi, wasingependwa na Mwenyezi Mungu. Tofauti kati ya Mtume na watu wengine sio kwamba yeye anatenda dhambi na Mwenyezi Mungu hata hivyo akampenda; bali ni kwamba yeye Mtume kamwe hatendi dhambi wakati watu wengine wanatenda. Huu ni ujumla ambao haukubali upekee. Kuhusiana na kipengele cha wakati pia, jambo hilo hilo linatumika. Je inaweza kusemwa kwamba jambo fulani linafungamana na wakati fulani? Kwamba Mwenyezi Mungu anawapenda madhalimu kwa wakati fulani, lakini baadaye akabadili mawazo Yake, akaifuta nafasi Yake ya awali, na akasema baadaye kwamba Yeye hawapendi madhalimu? Hapana, hili haliruhusu ubatilishaji.

Katika aya mojawapo ya jihadi Qur'ani inasema kwamba:

وَقَٰتِلُواْ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ ٱلَّذِينَ يُقَٰتِلُونَكُمۡ وَلَا تَعۡتَدُوٓاْۚ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُحِبُّ ٱلۡمُعۡتَدِينَ

**‘Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaowapiga, wala msichokoze. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wachokozi.” (Qur’an 2:190)**

Kwa wale wanaotupiga, kwa wale ambao wameanzisha aina fulani ya uchokozi dhidi yetu, hao tunapaswa kupigana nao. Lakini sisi wenyewe hatupaswi kuwa wachokozi. Kupigana dhidi ya uchokozi sio uvamizi. Lakini kupigana dhidi ya kingine kisichokuwa uchokozi au uvamizi huo ni uchokozi na sio halali. Tunapaswa kupigana dhidi ya uchokozi ili kuondoa uchokozi; lakini kama tutapigana dhidi ya kinginecho, basi sisi tutakuwa wachokozi. Hili sio jambo ambalo linakubali ubatilishwaji. Inawezekana kwa mfano, kwamba ruhusa kwa ajili ya jihadi na ulinzi binafsi ukazuiliwa kwa kipindi fulani kwa faida bora yetu wenyewe, kwa ajili yetu sisi kuvumilia na kustahimili kwa muda kiasi, halafu baadaye, wito wa jihadi unatolewa, ikiwa na maana kwamba ile amri ya kuwa na subira imefutwa kwa sababu ilikuwa ni kwa kipindi kilichokadiriwa tu. Ufutwaji wa amri hii ni kwa sababu kuanzia mwanzoni kabisa ilikusudiwa kuwa ya muda tu.

## ULINZI WA MAADILI YA UBINADAMU

Qur’ani inaweka mipaka ya jihadi hasa kwenye aina ya ulinzi na inairuhusu tu katika kukabiliana na uchokozi. Lakini katika mlango uliopita, tumesema kwamba jihadi kwa ajili ya upanuzi wa maadili ya binadamu, hata kama sio dhidi ya uchokozi, haiwezi ikashutumiwa. Tumesema pia kwamba maana ya uchokozi ni ya kijumla, ikiwa na maana kwamba sio lazima kwa uchokozi kuwa dhidi ya uhai, dhidi ya mali, dhidi ya utukufu, dhidi ya ardhi, dhidi ya uhuru na dhidi ya hiari. Kama kundi likifanya uchokozi dhidi ya manufaa ambayo yanahesabiwa kama maadili ya binadamu, basi huu ni uchokozi.

Napenda nitoe mfano rahisi. Katika zama zetu, juhudi kubwa zinafanywa kuelekezwa kwenye kung'oa magonjwa mbalimbali. Hadi sasa vyanzo au sababu za baadhi ya magonjwa kama saratani hazijagunduliwa bado, na tiba yao kadhalika bado haijajulikana. Lakini kwa sasa hivi, yapo madawa ambayo yanaweza kuchelewesha zile athari za magonjwa haya. Fikiria iwapo kwamba taasisi fulani inagundua tiba ya moja ya magonjwa haya, na kwamba taasisi nyingine ambazo zinanufaika na uwepo hasa wa ugonjwa huo, vile viwanda ambavyo vinatengeneza yale madawa ambayo yanaweza kutumika kuahirisha zile athari za huo ugonjwa, ili kukinga soko lao kutokana na kuporomoka – katika suala ambalo mamillioni, mabilioni ya dola yangepotea – wao wataharibu ile dawa mpya iliyogunduliwa ambayo ina manufaa sana; watawabomoa wale wanaohusika nayo; wataiharibu ile fomyula mpya ili kusiwe na mtu anayejua chochote kuihusu hiyo. Sasa, hivi thamani ya ubinadamu kama hiyo ni ya kutetewa ama laa, ni ya kuachwa vivi hivi tu? Je tunaweza kusema kwamba hakuna aliyeshambulia maisha yetu au mali zetu, hakuna aliyeingilia kwenye utukufu wetu, uhuru wetu au nchi yetu, lakini kwamba katika pembe moja ya dunia, mtu fulani amefanya ugunduzi na mtu mwingine tena anajaribu kuuharibu, na kujiuliza kwamba hilo linatuhusu nini sisi? Hapana. Hii sio nafasi ya swali kama hilo. Hapa thamani ya binadamu inatishiwa. Hivi sisi ni wa kuitwa wachokozi kama tukichukua hatua ya upinzani na vita? Hapana, sisi tumejitokeza kuupinga uchokozi na kupigana na hao wachokozi.

Kwa hiyo, tunaposema kwamba msingi wa jihadi ni ulinzi, hatumaanishi ulinzi kwa maana yenye mipaka ya kupaswa mtu kujilinda wakati anaposhambuliwa kwa upanga, bunduki au kwa mizinga. Hapana, tuna maana kwamba, kama nafsi ya mtu, thamani ya mali ya kiroho zinapochokozwa, au kwa kweli, kama jambo

ambalo mwanadamu analithamini au kuliheshimu na ambalo ni muhimu kwa ustawi na furaha ya mwanadamu linapochokozwa, hapo tunapaswa kulilinda.

Hapa tunarudi tena kwenye mjadala wetu uliopita kuhusu iwapo Tawhiid ni suala la kibinafsi au ni mojawapo ya maadili ya kibinadamu. Kama ni hili la maadili ya binadamu ambalo ni lazima lilindwe, kama miongoni mwa jumla ya sheria kuna moja ambayo inaamuru kwamba Tawhiid lazima ilindwe juu ya kanuni ya kuwa yenyewe ni manufaa ya msingi ya binadamu (kama katika Uislamu kwa mfano) hii haina maana kwamba uchokozi uonekane kuwa ni halali. Hii ina maana kwamba Tawhiid ni maadili ya kiroho na maana ya ulinzi ni pana kiasi kwamba inajumuisha vilevile na ulinzi wa maadili ya kiroho.

Hata hivyo, nitarudia tena kwamba Uislamu hausemi ni lazima tupigane kulazimisha Tawhiid, kwa vile Tawhiid ni jambo ambalo haliwezi kulazimishwa kwa sababu ni imani. Imani inajengwa juu ya utambuzi na chaguo, na utambuzi hauvutwi kwa nguvu. Hilo hilo linatumika kwenye chaguo la hiari: '*Hakuna kulazimisha katika dini'* ina maana kwamba tusiwalazimishe watu, kwani imani sio jambo ambalo linaweza kushurutishwa juu ya mtu. Hata hivyo '*'Hakuna kulazimisha katika dini*' haimaanishi kwamba hatupaswi kutetea haki za Tawhiid. Haina maana kwamba, kama tukiona kwamba '*Laillaha illa Allah*' – Hakuna mungu isipokuwa Allah inatishiwa kutoka upande fulani sisi tusiitetee na kuilinda.

## UHURU WA IMANI, FIKRA (MAWAZO)

Hapana shaka kwamba dini lazima isishurutishwe au kulazimishwa juu ya mtu. Watu lazima vilevile wawe huru katika uchaguzi wao

wa dini. Kwa maneno mengine, uhuru wa mawazo na uchaguzi ni tofauti na uhuru wa imani. Imani nyingi zinatambulika na kuonekana kuwa ni za kweli na zimechaguliwa kwa hiari. Kujiingiza na msimamo wa moyo wa mtu kwenye imani zake mara nyingi kunajengwa na utambuzi na uchaguzi. Lakini je, imani zote za binadamu zimejengwa juu ya fikira, utambuzi na uchaguzi? Au wingi wa imani za binadamu sio zaidi ya kujiingiza na kuwa na msimamo kwa nafsi ya mwanadamu kwenye mambo ya kisilika? Mfano unaotolewa na Qur'ani katika suala ya uigizaji wa kizazi kimoja kwenye kizazi kilichotangulia ni?

..... إِنَّا وَجَدْنَآ ءَابَآءَنَا عَلَىٰٓ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰٓ ءَاثَٰرِهِم مُّقْتَدُونَ ﴿٢٣﴾

**'.....Hakika sisi tuliwakuta baba zetu juu ya desturi na tunafuata nyayo zao....." (Qur'an 43:23)**

Qur'ani inaweka msisitizo mkubwa juu ya jambo hili, na inakuwa vivyo hivyo kwenye imani ambayo imeundwa kwa uigizaji wa waungwana wa jamii. Katika sehemu kama hizo, maneno uhuru wa imani hayana maana asilani, kwani uhuru una maana ya kukosekana kwa vipingamizi kwenye shughuli za nguvu hai na yenye kuendelea, ambapo aina hii ya imani ni namna ya kibano na udororaji. Uhuru katika kibano ni sawa na uhuru wa mfungwa aliyehukumiwa kifungo cha maisha, au uhuru wa mtu aliyefungwa nyororo nzito na tofauti pekee ni kwamba yule mtu ambaye amefungwa kimwili anaihisi hali yake, ambapo yule ambaye nafsi yake iko kwenye minyororo halitambui hilo. Hili ndio tunalomaanisha pale tunaposema kwamba uhuru wa imani, ulioegemea kwenye uigizaji na athari za kimazingira, badala ya uhuru wa fikira.

## JIZYAH (AINA YA KODI)

Jambo la mwisho la kujadili ni *Jizyah*, yaani aina ya kodi. Katika moja ya aya za Qur'ani imefunuliwa kwamba tunapaswa kupigana na Watu wa Kitabu bila masharti au wale ambao hawana imani ya kweli mpaka walipe *jizyah*. Ni nini *jizyah*? Je maana ya jizyah ni aina fulani ya 'pesa za ulinzi' au 'ushuru*?'* Je wale Waislamu waliokuwa wakichukua *jizyah* hapo zamani walikuwa wakichukua pesa ya ulinzi? Pesa ya ulinzi, kuangaliwa kutoka upande wowote ni dhulma na uonevu na Qur'ani yenyewe inaukana huo kwa muundo wowote ule. *Jizyah* inapata mzizi wake katika neno *Jaza*. Katika lugha ya Kiarabu neno *Jaza* linatumika pote, katika malipo na katika adhabu. Ikiwa *jizyah* katika muktadha huu ina maana ya fidia au adhabu, basi inaweza ikadaiwa kwamba maana yake ni 'pesa za ulinzi' au 'ushuru,' lakini kama ina maana ya malipo, ambayo ndio maana yake yenyewe, basi jambo hilo hubadilika.

Hapo kabla kidogo tulisema kwamba baadhi ya watu wamedai kwamba *jizyah* kimsingi sio neno la Kiarabu, kwamba lina asili ya Kiajemi, kwamba ni namna ya Uarabishaji – yaani muundo wa kulifanya neno kuwa ni la Kiarabu – wa neno la Kiajemi '*gaziyah*' jina la kodi ya kichwa ambayo ilianzishwa kwa mara ya kwanza na mfalme wa Uajemi aitwaye Anoushiravan, na kwamba wakati neno hili lilipokutana na Waarabu, ile herufi 'G' ilibadilishwa na kuwa 'J' kulingana na kanuni ya kawaida, ili kwamba Waarabu badala ya kusema 'gaziyah' wakaita '*jizyah*.' Hivyo *jizyah* lina maana ya kodi, na kulipa kodi sio sawa na kutwaa pesa kwa mabavu kwa ajili ya ulinzi. Waislam pia lazima walipe kodi na tofauti pekee iliyopo ni kati ya zile aina halisi za kodi ambazo Waislam wanapaswa kulipa na zile ambazo ni za kulipwa na Watu wa Kitabu. Hakuna uthibitisho hata hivyo juu ya maoni haya, kwamba asili ya neno hilo sio ya

Kiarabu, na zaidi ya hayo, hatuna umuhimu wa haraka katika neno hili. Vyovyote utakavyokuwa huo mzizi wa neno hilo, ambalo ni lazima tulifanye ni kutafuta sura asili ya *jizyah* kutoka kwenye sheria ambazo Uislamu umeziweka, na ambazo kwazo imefafanuliwa kivitendo.

Kuliweka katika njia tofauti, ni lazima tuangalie ili tuone iwapo Uislamu unaichukulia *jizyah* kuwa ni tuzo ama ni adhabu. Ikiwa kwa malipo ya *jizyah*, Uislamu unafanya shughuli fulani, unatoa huduma fulani, basi malipo ya *jizyah* ndio tuzo yake. Ikiwa hata hivyo unachukua *jizyah* bila ya kutoa chochote badala yake, basi ni aina ya pesa za ulinzi. Kama kuna wakati ambapo Uislamu unatuambia tuchukue *jizyah* kutoka kwa watu wa kitabu bila kutoa chochote badala yake, unatuambia tuchukue tu pesa kutoka kwao ama sivyo tuwapige, basi hizo ni pesa za ulinzi. Kuchukua pesa za ulinzi maana yake ni kuchukua haki ya kutumia nguvu. Ina maaana kwamba wale wenye nguvu wanawaambia wale ambao ni wanyonge watoe kiasi cha fedha kama wanataka waachwe walivyo na kama hawataki kuingiliwa au usalama wao kuvurugwa. Kama, kwa upande mwingine, Uislamu unasema kwamba unaweka shughuli fulani mbele ya Watu wa Kitabu na badala ya shughuli hiyo wao wanapaswa kulipa *jizyah* kwa Uislamu, basi katika hali hii, maana ya *jizyah* ni tuzo, iwe ni neno la Kiarabu ama la Kiajemi. Tunachopaswa kuzingatia ni ile sura asili ya sheria, sio asili ya neno.

Tunapoelewa msingi wa sheria hii, tunagundua kwamba *jizyah* ni kwa ajili ya lile kundi la Watu wa Kitabu wanaoishi chini ya ulinzi wa dola ya Kiislamu, ambao wanategemea hiyo dola ya Kiislamu. Dola ya Kiislam ina wajibu fulani kwa umma na hivyo huo umma nao una wajibu wa kiheshima kwa dola ya Kiislamu, na wa kwanza kati ya wajibu hizo ni kulipa kodi ili kuiwezesha bajeti ya dola. Kodi hizi zinajumuisha *Zaka* na zile ambazo ziko katika muundo

wa kodi mbalimbali ambazo Dola ya Kiislamu inazianzisha kwa mujibu wa maslahi bora ya Kiislamu. Kodi zote hizi lazima zilipwe na watu wenyewe. Iwapo hawatalipa, basi serikali hiyo ya Kiislam haitaweza kufanya kazi na kujiendesha yenyewe. Hakuna bajeti ya serikali ambayo haipewi fedha zote ama sehemu yake na watu wake. Serikali yoyote, ili iwe na bajeti, lazima iipate ama moja kwa moja, ama kwa njia za mzunguko kwa kodi.

Wajibu au kazi ya pili ya raia ni kutoa askari kuchukua shughuli ya kujitoa mihanga kwa ajili ya taifa. Zinaweza zikawepo hatari za baadaye ambapo raia wa nchi hiyo ni lazima wasaidie katika ulinzi. Kama hao Watu wa Kitabu wanaishi chini ya ulinzi wa serikali hiyo ya Kiislamu, wao hawalazimiki kulipa hizo kodi za Kiislamu na wala hawalazimiki kushiriki katika jihadi hiyo, ingawaje hata hivyo, manufaa yoyote yatakayopatikana kutokana na jihadi hiyo yatawanufaisha na wao pia. Kulingana na kanuni hii, wakati serikali hiyo ya Kiislamu inapoupata usalama wa watu na ukawaweka chini ya ulinzi wake, iwe ni watu wake wenyewe au hapana, inahitaji kitu fulani badala yake kutoka kwao, kifedha ama vinginevyo. Kutoka kwa Watu wa Kitabu, badala ya *Zaka* na kodi nyinginezo za Kiislamu, serikali hiyo inahitaji hiyo *jizyah* na vile vile badala ya askari, itahitaji hiyo *jizyah*. Katika mwanzoni mwa Uislamu, wakati wowote Watu wa Kitabu walipojitolea kuja kupigana katika safu za Waislamu, kwa maslahi ya dola hiyo ya Kiislamu, Waislamu hawakukusanya *jizyah* kutoka kwao. Katika Tafsiri ya Qur'ani inayoitwa '*Tafsir al-Manar*,' kuna maelezo mengi kutoka kwenye vitabu mbalimbali vya historia ya jinsi Waislamu wa mwanzoni walivyokusanya *jizyah* badala ya askari, na jinsi Watu wa Kitabu walivyokuwa wakiambiwa kwamba kwa vile walikuwa wakiishi chini ya ulinzi wa serikali ya Kiislamu na chini ya Waislamu wenyewe lakini hawatumi askari (Waislamu wenyewe wasingekubali askari wao), basi badala ya kutuma askari,

wao walipaswa kulipa *jizyah*. Na endapo katika wakati mmoja, Waislamu katika hali fulani walipata uaminifu juu yao na wakakubali askari wao, basi hawakuchukua tena hiyo *jizyah* kutoka kwao.

Kwa hiyo, kutoka kwenye maana yake ya kisheria, *Jizyah* ni tuzo kwa serikali ya Kiislalmu kutoka kwa raia wake Watu wa Kitabu wasiokuwa Waislamu, kwa marejesho kwa ajili ya huduma inazowafanyia na mbadala wa wao kutopaswa kuipatia dola hiyo askari na kwa kutokuwa na kulipa kodi.

Sasa suala la kwanza la vipi na kwa nini Uislam unaacha jihadi yake kwa ajili ya *Jizyah* linakuwa linaeleweka wazi. Jawabu linatolewa na swali la: 'Kwa nini Uislamu unataka Jihadi?" Hautaki jihadi kwa ajili ya kushurutisha imani yake bali unataka jihadi kwa ajili ya kuondoa vikwazo. Wakati huo upande mwingine unatuambia sisi kwamba hauna madhumuni ya kupigana na sisi na kwamba hautaweka kikwazo kwenye wito wa Tawhiid, na utaliheshimu neno lake la ahadi, basi inapaswa kuamuliwa kulingana na aya hii:

۞ وَإِن جَنَحُواْ لِلسَّلۡمِ فَٱجۡنَحۡ لَهَا

**'Na kama wakielekea kwenye amani, nawe ielekee....."**

Kama wamenyenyekea na kuonyesha mawazo na moyo wa amani na maelewano, basi hatupaswi kuwa wakali tena. Hatupaswi kusema: **'Oh, hapana. Sisi hatutaki amani, bali tutapigana."**

## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana

39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)

81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102 Hukumu zinazomhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru

123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur’an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur’an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur’ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu

165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam 'Ali ('a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja'aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Mjadala wa Kiitikadi

206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Mwanamke na Sharia
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahjul-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
223. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
224. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
225. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
226. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
227. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi
228. Qur'ani na Kuhifadhiwa Kwake
229. Shia na Qur'ani – Majibu na Maelezo

## KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique